epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Jumanne Oktoba 15, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581828
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22

**TCHOUAMEN HANA MPANGO NA LIVERPOOL**

UKURASA WA 2

**HATIMA YA 'AFANDE' KESI YA BINTI WA YOMBO LEO**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Dodoma leo inatarajiwa kutoa uamuzi wa maombi ya Wakili Peter...

UKURASA WA 3

**WATAKA UMAKINI UANDIKISHAJI UCHAGUZI S/MITAA**

VIONGOZI mbalimbali wamewataka waandikishaji wa wapigakura katika Daftari la Wakazi kuwa...

UKURASA WA 18

**ASKOFU: ANAYEBEZA MAENDELEO NCHINI AKAMWULIZE MAMA YAKE MZAZI**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Mwanza, Mhashamu Renatus Nkwande, amewataka Watanzania...

**Kutoka 1934 Malecela ana mazito haya**



UKURASA 9&10

## KAMANDA MSSIKA

# Kutoka fundi gereji hadi msaidizi IGP



• **Miaka** 40 jeshini; mtihani kumchunguza kachero, mwasisi Kanda Maalum ya Dar, moto wa vitani Kagera... *Endelea ukurasa 4*



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea Mwenge wa Uhuru kutoka kwa kiongozi wa mbio hizo kitaifa, Godfrey Mzava wakati wa kilele cha maadhimisho ya Mbio za Mwenge wa Uhuru kwenye Uwanja wa CCM Kirumba, jijini Mwanza jana. **PICHA: IKULU**

# Samia: Tusiuchukulie poa Uchaguzi Serikali za Mitaa

UKURASA 2

**MICHEZO** **TAIFA STARS NI KUFA, KUPONA LEO** UK.24 **KATUNI** UK.6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akishiriki Ibada ya Misa Takatifu ya Kumbukizi ya Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere pamoja na viongozi wengine; Katibu Mkuu wa CCM, Balozi Dk. Emmanuel Nchimbi (kushoto), Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi (wa pili kushoto) na Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa, iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mtakatifu Francis Xavier, Nyakahoja jijini Mwanza jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Samia ataka uchaguzi Serikali za Mitaa usichukuliwe poa

**Na Vitus Audax,** MWANZA

RAIS Samia Suluhu Hassan amewataka Watanzania kutokuchukulia poa uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Novemba 27, mwaka huu na kuwa ndio utaleta taswira nzima ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Mwanza wakati wa maadhimisho ya kilele cha Mbio za Mwenge wa Uhuru na kueleza ni fursa kubwa ya kukuza demokrasia na ushiriki katika maendeleo ya jamii.

"Kama vijana wanavyosema 'tusiuchukulie poa' ni uchaguzi kama uchaguzi mwingine, ni uchaguzi unaotupa taswira jinsi mambo yatakavyokuwa kwenye uchaguzi mkuu wa 2025 hivyo niendelee kuwasihi wananchi wote wenye sifa kuhakikisha wanashiriki kwenye uchaguzi huu muhimu," alisema Samia.

Aliwataka kutofautisha kati ya orodha ya wapigakura inayotumika katika kupiga kura uchaguzi wa serikali za mitaa (Daftari la Wakazi) pamoja na Daftari la Kudumu la Wapigakura ambalo hutumika katika uchaguzi mkuu mwakani.

"Niwaombe na kuwahimiza wananchi wote twende kwenye maeneo yetu tukajiandikishe, ili kushiriki uchaguzi ujao kwani utasaidia kuonesha ushiriki wa wananchi katika maendeleo ya maeneo yao sambamba na kubuni, kusimamia na kutekeleza shughuli za kiuchumi katika ngazi ya jamii kwa maendeleo jumuishi ya watu katika maeneo husika ya kiutawala," alisema Samia.

Aidha, alisema msingi wa kuwapo kwa ngazi za kiutawala kikatiba katika mikoa, wilaya, miji na vijiji ni kupeleka madaraka kwa wananchi na ughatuzi huo wa madaraka unaongeza ushiriki wa wananchi katika maamuzi ikiwa ni dhana ya kujitawala.

### MAZINGIRA

Kuhusu uharibifu wa mazingira, Rais Samia alisema hali ya uchafuzi imekuwa tatizo nchini pamoja na ulimwenguni kwa pamoja hali inayosababisha athari zake kurejea kwa kasi.

"Athari za uchafuzi au uharibifu wa mazingira zinaturudia sisi wenyewe kwa kutokea kwa mabadiliko ya tabianchi na misimu ya mvua na jua mabadiliko yanayosababisha upungufu wa mvua pamoja na mvua kupita kiasi, mvua zisizotabirika na ukame katika baadhi ya maeneo ya nchi vyote hivi vinaleta dhiki kwetu au kwa wananchi.

Kadhalika, alisema maeneo yote yaliyolalamikiwa katika mbio za Mwenge serikali itayafanyia kazi sambamba na maoni na mapendekezo ya wakimbiza mwenge kitaifa.

Kuhusu uzinduzi wa kitabu cha historia ya falsafa ya Mwenge wa Uhuru alichokizindua jana, Rais Samia alisema kitabu hicho kitasaidia kueneza na kutunza na kuendeleza historia na misingi ya Mbio za Mwenge pamoja na mchango wa vijana katika shughuli hizo.

Awali, akitoa taarifa ya Mbio za Mwenge Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Ridhiwani Kikwete, alisema Mwenge huo umekimbizwa kwa zaidi ya kilomita 37,235.62 katika mikoa 31, halmashauri 195 kwa siku 195 ukiongozwa na vijana sita wawili kutoka Zanzibar, Kigoma, Kilimanjaro, Dar es Salaam huku kiongozi wa mbio hizo akitokea mkoani Mwanza.

### MAENEO KOROFI

Akitoa ripoti ya mbio za Mwenge kitaifa, Kiongozi wa Mbio hizo, Godfrey Mzava alitaja maeneo matatu korofi yaliyobainika wakati wa mbio hizo huku akimwomba Rais Samia Suluhu Hassan kuyatilia mkazo ikiwezekana yaangaziwe maeneo hayo pekee katika mbio zijazo.

Alitaja maeneo hayo kuwa ni pamoja na tatizo la ukataji wa kodi za serikali katika fedha za serikali zinazotolewa kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

"Viwango vya kodi hizi vinajulikana na ni kwa mujibu wa sheria lakini mamlaka husika hazitimizi wajibu wake wa kuhakikisha zinakatwa na kurudishwa TRA. Changamoto hii imekuwa ikiibuliwa na Mwenge wa Uhuru na imekuwa ikijitokeza katika miradi mingi inayotekelezwa hapa nchini hili ni eneo la kufuatilia kwa makini," alisema Mzava.

Aidha, alitaja zabuni za miradi mingi ya umma kuwa zinazotolewa nje ya mfumo wa kidigitali wa manunuzi ya umma (NeST) hatua ambayo ni kinyume cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2023 pamoja na Sheria ya Ubadhirifu wa Mali ya Umma na Utoaji wa Zabuni za Umma usiyo ridhisha.

Kadhalika, alitaja eneo lingine kuwa ni pamoja na halmashauri nchini kushindwa kutumia mapato ya ndani kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo na kuishia kutegemea fedha kutoka serikali kuu na taasisi za umma.

Mzava alisema ni halmashauri chache tu nchini zinazotekeleza miradi ya maendeleo kwa wananchi kwa kutumia fedha za ndani. Aidha, alisema halmashauri nyingi hazina maelezo yanayoridhisha kuhusu matumizi ya fedha za mapato ya ndani wanayokusanya hasa katika eneo hilo la utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi.

"Ikitokea Rais akaelekeza kuwa mbio za Mwenge wa Uhuru wa mwaka 2025 zishughulikie miradi inayotekelezwa na mapato ya ndani ya halmashauri zetu hapa nchini, watu watakimbia halmashauri zao," alisema Mzava.

Aidha, alimwomba Rais kuelekeza kwa mwaka 2025 Mwenge wa Uhuru ushughulike na miradi inayotekelezwa na mapato ya ndani ya halmashauri nchini. Suala lingine alilolitaja kuwa korofi ni pamoja na usambazaji wa nishati vijijini chini ya usimamizi wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) na kueleza kuwa utekelezaji wake ni kero katika maeneo mengi nchini na kuomba pia eneo hilo kupewa kipaumbele zaidi katika ufuatiliaji.

"Ukielekeza hivi Rais utashuhudia maendeleo makubwa ya watu kwa muda mfupi kupitia Mwenge huu wa uhuru na itakuwa ni hatua muhimu katika kuunga mkono jitihada unazozifanya katika kujenga nchi kupitia serikali kuu kwa kishindo kikubwa saana," alisisitiza na kukabidhi kitabu cha majumuisho ya risara za maeneo yote ulipozunguka Mwenge huo wa uhuru.

Pamoja na mambo mengine Rais Samia Suluhu Hassan alishiriki ibada ya kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha Hayati Mwalimu Julius Nyerere, alitembelea na kukagua maonesho ya wiki ya vijana yaliyohitimishwa katika viwanja vya Furahisha pamoja na kuzindua kitabu cha Falsafa ya Mwenge wa Uhuru kilichoandikwa na miongoni mwa mawaziri wa kwanza Tanzania, Job Lusinde na kuhaririwa na Dk. Bashiru Ally.

BINTI WA YOMBO

# Hatima ya 'afande' kujulikana leo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MAHAKAMA ya Wilaya ya Dodoma leo inatarajiwa kutoa uamuzi wa maombi ya Wakili Peter Madeleka ya kukamatwa na kuwekwa rumande Fatma Kigondo, maarufu afande, mshtakiwa katika kesi ya kuwatuma vijana kumbaka na kumwingilia kinyume cha maumbile binti mkazi wa Yombo Dovya, Dar es Saalam.

Hatima ya mshtakiwa huyo inatarajiwa kujulikana leo kama mahakama hiyo itatoa amri ya kukamatwa kwake na kuwekwa rumande kama ilivyokuwa kwa washtakiwa wengine kwa ajili ya usalama wake.

Wakili wa upande wa mlalamikaji Peter Madeleka alitoa maombi hayo Oktoba 7 mwaka huu katika Mahakama ya Wilaya Dodoma.

Madeleka aliomba mahakama hiyo kutoa amri ya kumkamata na kumweka rumande mshtakiwa huyo kwa ajili ya usalama wake kama ambavyo ilifanya kwa washtakiwa wengine.

Fatma anakabiliwa na shtaka la kubaka kwa kundi kinyume cha kifungu cha 131 A (2) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu, Sura 16, ambacho kinaelekeza kuwa ni kosa kisheria kuwasaidia wahalifu kutenda kosa la ubakaji, afande huyo akidaiwa anahusika na ukatili wa ubakaji wa kundi. Kesi hiyo ambayo ilipangwa kusikilizwa Oktoba 7, mwaka huu, lakini iliahirishwa hadi leo baada ya mshtakiwa kutofika mahakamani kwa madai kuwa ni mgonjwa.

Wakili Madeleka akiwasilisha maombi hayo mbele ya Hakimu Mkazi wa Mwandamizi wa Mahakama ya Wilaya ya Dodoma, Nyambuli Tungaraja, akidai mahakama itoe amri ya kukamatwa kwa Fatma na kumwekwa rumande katika Gereza la Isanga jijini hapa.

Wakili Madeleka alidai anaiomba mahakama hiyo kutoa amri hiyo ili mshatakiwa huyo akamatwe mara moja na kunyimwa dhamana kama ilivyokuwa kwa washtakiwa wengine.

Wakali wa Mlalamikiwa, Sedrick Mbunda alidai mteja wake hakufika mahakamani kutokana na kuwa mgonjwa na kuiomba mahakama impangie siku nyingine ya kusikiliza shauri hilo.

Ni hoja iliyopingwa na Wakili Madeleka ambaye alihoji kuwa kama mshtakiwa huyo ni mgonjwa, kwanini wakili huyo hakuwasilisha ushahidi wa daktari mbele ya mahakama hiyo.

"Kama anaumwa lazima wangeleta ushahidi wa daktari kama ambavyo wanatakiwa kufanya kwa mujibu wa sheria, lakini hii kusema tu mtu anaumwa, si kazi ya mahakama kubaini kama mtu anaumwa kweli au haumwi, walipaswa kuleta ushahidi wa kimatibabu hapa si kuzungumza tu," alidai Wakili Madeleka.

Hakimu Tungaraja aliahirisha shauri hilo hadi leo kwa ajili ya hoja hizo kutolewa uamuzi.

## HABARI KITAIFA



Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) na Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, akifungua rasmi Mkutano Mkuu wa 149 wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU) uliofanyika katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha CICG, Geneva nchini Uswisi jana. **PICHA: BUNGE**

# Viongozi wataka umakini uandikishaji serikali za mitaa

**Na Waandishi Wetu**

VIONGOZI mbalimbali wamewataka waandikishaji wa wapigakura katika Daftari la Wakazi kuwa makini na utambuzi wa Watanzania ili kuepuka uwezekano wa kuandikisha wasio raia.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Shinyanga, Morogoro na Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, mkoani Rukwa wakati wakijiandikisha kwenye mitaa yao, walisema kila Mtanzania ana haki ya kushiriki uchaguzi huo na ni muhimu kutumia vyema nafasi hiyo.

**SHINYANGA**

Juzi Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amejiandikisha kwenye daftari la wakazi katika viwanja vya Ikulu Manispaa ya Shinyanga, huku akionya kuandikisha watu ambao sio raia wa Tanzania.

Akizungumza baada ya kujiandikisha kwenye daftari hilo, alitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kujiandikisha ili wapate fursa ya kupiga kura Novemba 27 na kuchagua viongozi wazuri ambao watawaletea maendeleo.

**RUKWA**

Serikali wilayani Kalambo mkoani Rukwa imewaonya baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo kuacha kuwapokea na kuwapa hifadhi watu wanaoingia nchini kwa njia za panya.

Aidha, alisema kwa kufanya hivyo kuna uwezekano mkubwa wa kuathiri uandikishaji wa wakazi kwenye Daftari la Wakazi kwa ajili ya kupiga kura kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Mkuu wa Wilaya ya Kalambo, Dk. Lazaro Komba alisema kuwa wilaya hiyo inapakana na nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo pamoja na Zambia ambako wananchi kutoka mataifa hayo wamekuwa na tabia za kutembeleana wakiamini kuwa ni ndugu.

Alisema wananchi hao wanafanya kosa la kisheria kuwapokea wageni hao na kuwapa hifadhi na wanatakiwa kuacha mara moja, kuingia nchini hawazuiliwi isipokuwa wanapaswa kufuata taratibu za kisheria. Alisema wakiachwa waingie nchini kinyemela wanaweza hata kujiandikisha katika Daftari la Wakazi wa serikali za mitaa na wakawachagulia wananchi viongozi ambao hawakuwataka.

Aidha, ni jukumu la kila mwananchi wa wilaya hiyo kutoa taarifa za mgeni katika kijiji chake ama kitongoji, na pia akimwona katika maeneo ya kuandikisha orodha ya wapigakura ili vyombo vya usalama vichukue hatua mara moja.

**MTWARA**

Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Patrick Sawala, akizindua uandikishaji wakazi katika Mtaa wa Shangani East, alisema ameridhishwa na mwitikio wa wananchi, akitoa wito kwa viongozi wa jamii kuendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kujiandikisha.

"Leo tunaanza zoezi la uandikishaji kuelekea uchaguzi huu. Nimeungana na wananchi kujiandikisha, na ninatoa wito kwa kila mmoja ajitokeze kwa wingi," alisema.

Mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Stella Maris, Juma Omari, alisisitiza umuhimu wa vijana kushiriki kwa kuwa ni haki ya msingi na wajibu wao kujiandikisha.

Mwanafunzi wa Chuo cha Ualimu, Hawa Sule, alihimiza vijana wa kike kujitokeza kujiandikisha na kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali.

Mkazi wa Shangani West, Zamda Jafari, ameonesha wasiwasi kuhusu mwitikio wa wanawake kujiandikisha.

**MOROGORO**

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima, alionya viongozi wa vyama vya siasa, makundi ya watu na viongozi wa kijamii wenye nia ovu ya kushawishi au kuharibu uandikishaji kwa ajili ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kuwa wasithubutu na kwamba hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

Alisema hakuna kiongozi wa chama chochote au mtu yeyote mwenye mamlaka ya kumzuia mwenye sifa ikiwamo ya umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea kujiandikisha kwa kuwa ana haki ya kushiriki na kuchagua kiongozi anayemtaka kwenye uchaguzi huo wa serikali za mitaa.

"Nasisitiza asitokee kiongozi yeyote awe wa kisiasa, kijamii, dini au mtu yeyote kumzuia au nia ovu ya kukwamisha zoezi hili la uandikishaji kwenye daftari kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa," alisema Malima.

Uandikishwaji wapigakura katika Daftari la Wakazi ulizinduliwa Oktoba 11, 2024 na Rais Samia Suluhu Hassan katika Kijiji cha Chamwino Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma.

***Imeandikwa na Gurian Adolf (KALAMBO), Baraka Jamali (MTWARA) na Ashton Balaigwa (MOROGORO)***


## DAR RAPID TRANSIT AGENCY

DART
DAR RAPID TRANSIT

## Request for Expression of Interest to Invest in Transit-Oriented Development (TOD) at Gerezani BRT Terminal in Dar es Salaam.

The **Dar Rapid Transit (DART) Agency** is a governmental entity established by **Government Notice (GN) No. 120 of 25th May 2007 under the Executive Agencies Act No. 30 of 1997.** The Agency's mandate is to **plan, develop, and manage an efficient public transport system** in Dar es Salaam to reduce traffic congestion, promote sustainability, and improve urban mobility.

1. The Agency owns a parcel of land in a prime area located at Gerezani, Ilala District in Dar es Salaam, measuring approximately a total of 19,000m2, which is planned for accommodating **TRANSIT-ORIENTED DEVELOPMENT(TOD). The area is divided into two lots:**
   a) Lot One: 8,000 square meters
   b) Lot Two: 11,000 square meters
2. Developers may express interest in developing either one or both lots. Each lot must be submitted separately but under the same conditions and address.
3. The objective is to transform the Gerezani BRT Terminal into a more appealing customer-oriented hub to complement the transport services with them, but not limited to: -
   i. **Supermarkets**
   ii. **Retail Shops/Stores**
   iii. **Malls**
   iv. **Residential and**
   v. **Small Traders (Machinga)**
   vi. **Parkings**
4. To foster BRT services, the Agency plans to develop the referred piece of land under a Joint Venture model in a form to be agreed upon by both parties (investors).
   Therefore, the Agency seeks an eligible, reputable, competent investor(s) who powerfully demonstrates the appropriate muscles, experience, and expertise in designing and investing in the referred TOD at Gerezani BRT Terminal.
5. The developer may express interest in a Joint Venture (JV), but the JV must still meet all legal and technical requirements, with defined roles and responsibilities for each member.
6. This advert serves to invite sealed submission of the Expression of Interest from eligible and reputable investors to formally express their interest in investing in the referred TOD at Gerezani BRT Terminal under the Joint Venture or Design, Build, Finance, Operate/Maintain and Transfer **(DBFOMT)** Arrangements.
7. Those who are interested and find themselves to be eligible for investing in the referred TOD MUST avail the Agency with the following paper qualifications: -
   i. Expression of Interest letter
   ii. Company Profile
   iii. Document establishing the company (certified copies)
   iv. Pre-proposal design
   v. Feasibility study/business plan
   vi. Proposed financing model
   vii. Cost estimates
   viii. Audited Financial Statement for the past three (3) years
   ix. Profit-Sharing Proposal
   x. Proof of experience investing in a similar large-scale project for at least **Seven (7) years** worth at least **Tsh 100 billion.**
8. Expression of Interest MUST be accompanied by a proof of availability of funds for the proposed TOD project in either form from the reputable financing institution(s)
9. **NOTE:** This is not an invitation to tender
10. Interested investors who may wish to visit the area for the proposed TOD are humbly encouraged to do so and should contact the responsible Officer via Mobile No. +255 784632208 effectively from 16th October, 2024 to 30th October 2024.
11. A request for clarification MUST be in writing and reach the office of the undersigned at the latest five (5) days before the deadline for submission of the expression of interest.
12. The Agency has the mandate to accept or reject any submission and, if necessary, may annul the entire expression of interest process at any time without consideration for the interested investors.
13. Expression of interest in a sealed envelope marked **"EXPRESSION OF INTEREST FOR TRANSIT ORIENTED DEVELOPMENT (TOD) AT GEREZANI BRT TERMINAL** must be submitted on or before 30th October 2024 and should be either physically or electronically delivered to the address below:

**Chief Executive**
**Dar Rapid Transit Agency,**
**Ubungo Maji, Morogoro Road,**
**P.O. Box 724,**
**DAR ES SALAAM, Tanzania.**
**Email: ce@dart.go.tz**

## KAMANDA MSSIKA

# Kutoka fundi gereji hadi msaidizi wa IGP

**Na Romana Mallya**

MARUFUKU kukata tamaa! Jaribu kufikiria kuhusu hili: Alianzia kwenye mafunzo ya ufundi gereji, juhudi zake katika safari ambayo hakuwa na uhakika wa hatima yake, zikambeba hadi kuwa afande mwandamizi katika Jeshi la Polisi, hata kuwa Msaidizi wa Mkuu wa jeshi hilo, Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP).

Kamanda Abdallah Mssika aliyelitumikia Jeshi la Polisi kwa miaka 40 akishika nyadhifa mbalimbali, leo anasimulia milima na mabonde aliyopitia maishani tangu akiwa na umri wa miaka 15 hadi kustaafu kwake jeshini.

Kamanda Mssika aliwahi kuwa Mkuu wa Polisi (OCD) Wilaya ya Kinondoni, Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mara, Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Mwanza na Mkuu wa Upelelezi Mkoa wa Dodoma. Mstaafu huyo aliyewahi kuwa Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, pia Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, ni miongoni mwa makamanda waanzilishi wa Kanda Maalum ya Dar es Salaam mwaka 2006.

Pia amewahi kuwa Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera na baadaye kuwa Msemaji Mkuu wa Jeshi la Polisi hadi alipostaafu utumishi kwa umri wa lazima mwaka 2010.

Katika mazungumzo maalum na mwandishi wa habari hii yaliyofanyika Septemba 15 mwaka huu, mkoani Dar es Salaam, Kamanda Mssika anasimulia alivyoshindwa kuendelea na elimu ya sekondari baada ya baba yake kufariki dunia.

Anasema kifo cha baba yake kilibadili safari yake kimasomo, mama yake mzazi akilazimika kumpeleka kwa Mkuu wa Wilaya wa Iringa Mjini ili kumwomba msaada.

Ilikuaje? Kamanda Mssika anasema kuwa tofauti na watoto wengine, katika utoto wake hakuwahi kufikiria angetamani kuwa nani akiwa mkubwa.

"Nimesoma shule mbili hadi kuhitimu darasa la nane. Nilianza masomo Shule ya Ilole na baadaye kumalizia Shule ya Malangali, Iringa.

"Nikiwa darasa la sita, baba yangu alifariki dunia na kwa msaada wa kaka yangu mkubwa (Adam Mssika) nilihamishiwa Shule ya Malangali na kumaliza darasa la nane. Sikuendelea sekondari.

"Nikiwa na umri wa miaka 15, mama yangu alinichukua na kunipeleka kwa DC (Mkuu wa Wilaya) kumwomba msaada kwa sababu sina baba, anisaidie kuendelea sekondari au anitafutie kitu cha kufanya," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema kuwa baada ya kumpeleka kwa DC, mama yake aliondoka na hivyo Mkuu wa Wilaya alikwenda kumkabidhi kwa fundi mkuu katika moja ya gereji iliyokuwa mjini Iringa wakati huo, ili kujifunza ufundi. Alikaa hapo hadi mwaka 1966 alipokimbilia Dar es Salaam.

### MSHAHARA SH. 166

Anasema alipofika Dar es Salaam, alifikia kwa ndugu yake na katika kipindi cha mpito cha kutafuta ajira, alikwenda kujiandikisha Idara ya Kazi na mwezi Agosti mwaka huo (1966), alipata ajira ya muuguzi msaidizi katika Hospitali ya Muhimbili kwa mshahara wa Sh. 166.



Kamanda Abdallah Mssika akiwa kwenye mwonekano tofauti.



**Nikiwa na umri wa miaka 15, mama yangu alinichukua na kunipeleka kwa DC (Mkuu wa Wilaya) kumwomba msaada kwa sababu sina baba, anisaidie kuendelea sekondari au anitafutie kitu cha kufanya.**

"Nilifanya kazi wodi ya Kibasila. Nilifanya pale hadi mwaka 1970 na wakati wa likizo nikiwa Moshi, Kilimanjaro kwa kaka yangu Adam ambaye alikuwa trafiki, alinishawishi kuacha kazi ya uuguzi ili kuingia Jeshi la Polisi.

"Haikuwa kazi rahisi kuacha uuguzi kisha kwenda polisi kwa sababu tayari nilikuwa nimepata mafunzo ya uuguzi na nilikuwa katika hatua ya kubadilishiwa nafasi ya awali.

"Alimshirikisha pia baba yetu mdogo ambaye naye alinieleza umuhimu wake, ndipo Machi 17, 1970, nilijiunga rasmi Jeshi la Polisi na kupata mafunzo Chuo cha Usalama (Chuo cha Polisi Moshi - CCP).

Kamanda Mssika anasema kuwa baada ya kuhitimu mafunzo, alipangiwa mkoani Arusha na kuanza kazi za doria, kipindi hicho matukio makubwa yalihusisha wizi wa majumbani na mengine yaliyokuwa yakichunguzwa na ofisi za upelelezi.

Anasimulia kuwa baadaye alihamishiwa Dar es Salaam na miongoni mwa kazi alizofanya ni pamoja na kuwa dereva, akifanya kazi kama msaidizi.

"Nikiwa dereva, wakati maofisa wa polisi upelelezi wa makosa ya wizi wa kalamu au kughushi walikuwa wakitoka kwenda kufanya kazi zao, niliambatana nao.

"Yote niliyokuwa ninafanya sikuwa na uelekeo, lakini kupitia fursa mbalimbali zilizokuwa zinakuja mbele yangu na nikiangalia nilikotoka, nikawa ninaona ni nguvu zangu mwenyewe kunipeleka ninakotaka.

"Kulinganisha Dar es Salaam na Arusha nilikoanzia kazi, ofisi hii ilikuwa inashughulika na uhalifu wa aina zote. Wizi wa kalamu, matukio yalikuwa mengi wakati ule.

"Hivyo, nilivyokuwa nikitoka na wapelelezi wakifika eneo la tukio, badala ya kuwasubiria kwenye gari, nilipenda kuambatana nao, wanapohoji ninasikiliza, wakiandika maelezo ya mashahidi ambayo niliona ni rahisi kuliko ya watuhumiwa, nilikuwa ninaangalia hivyo ikafika wakati nikawa ninapewa fursa ya kuandika maelezo ya mashahidi," anasema.

Kamanda Mssika anasema kitendo hicho kilimpa uzoefu kujua wapi anakosea ili kurekebisha na mwaka 1975, alihamishwa kutoka Ofisi ya Mpelelezi Mkoa kwenda Makao Makuu ya Upelelezi na majukumu mengine yakawa kitengo cha makosa ya binadamu na vitendo vinavyohusisha wizi.

### KESI YA UHAINI

Kamanda Mssika anasema kutokana na uzoefu mkubwa aliopata, mwaka 1976 kulitokea kesi ya kwanza ya aina yake iliyomhusu mtendaji mwandamizi wa ulinzi na usalama wa nchi, Juma Thomas Zangira, aliyedaiwa kusaliti taaluma yake na nchi.

"Nikiwa makao makuu ya upelelezi, niliitwa na viongozi wangu wakuu na kunijulisha kwamba, nimeteuliwa katika timu ya wapelelezi Idara ya Usalama ya Taifa, ikiwa imeandaa operesheni maalum ya kumfuatilia tabia na mwenendo wa Zangira.

"Wakati huo nilikuwa kijana mwenye umri wa miaka 26 tu. Nipo Idara ya Upelelezi na cheo cha sajenti na ni mpenzi wa filamu hasa za kiupelelezi James Bond. Umeaminiwa na kupewa kazi hiyo, unakula kiapo mbele ya jopo.

"Sikufika sekondari, lakini katika utumishi wangu ndani na nje ya Jeshi la Polisi baada ya kustaafu, nimeingia katika taasisi ninapewa majukumu nyeti kupitiliza.

"Ilibidi kumfahamu mtuhumiwa anakaa wapi, alikuwa Mtaa wa Nkurumah (Dar es Saalam). Operesheni ikaanza, ikabainika mawasiliano, alikuwa anatoa siri akiwa ofisa mpelelezi wa juu aliyefunzwa kutoka taasisi mbalimbali za kiusalama nchi mbalimbali na ni kachero.

"Alikuwa ameandaliwa ofisi ya kuendesha majukumu yake ya kazi, ilikuwa (anataja moja ya hoteli kubwa iliyoko katikati ya jiji la Dar es Salaam)," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema kuwa wakati huo kulikuwa na matatizo ya kampeni ya ukombozi nchi za kusini mwa Afrika na Tanzania ikiiongoza.

"Wengi walitaka kujua siri, namna Tanzania inavyofanya, ndio wakampata yeye (Zangira) na akawa anafanya kazi hiyo.

"Operesheni iliyofanyika ilikuwa ni mwendelezo kujua nini kinachofanyika? Nani anakifanya? Anakifanyaje? Akishirikiana na nani? Na kina nani?" anasema.

### IDI AMINI

Kamanda Mssika anasema moja ya matukio yaliyotokea akiwa mafunzoni Chuo cha Polisi Kurasini, Dar es Salaam, wakati huo wakiwa likizo, Rais akatangaza wanaingia vitani, wakiwamo askari polisi.

"Tulitangaziwa tukarudi chuoni, ndipo tukakuta magari ya kutupeleka vitani. Amri ni utii. Tukatoka Dar es Salaam hadi Monduli, Arusha, tukapata mafunzo ya medani kivita ndipo hatimaye tukapelekwa mstari wa mbele tukianza Kagera na hatimaye kuvuka mpaka kuingia Uganda.

"Mimi baada ya kufika Monduli na kwenda Kagera, nilikuwa kikosi ambacho hatimaye nilibidi nichukuliwe na kuwekwa kitengo cha intelijensia kwa kuangalia wasifu wangu wa kufanya kazi katika ofisi za upelelezi za wilaya, mikoa na hali kadhalika Makao Makuu ya Upelelezi Tanzania (DCI)," anasimulia.

Kamanda Mssika anasema alikwenda na wasifu ambao ulimwaminisha kutoka kuwa askari wa miguu wa kawaida na kuingia kitengo hicho kama Msaidizi wa Mkuu wa Intelijensia wa Kikosi.

Anasimulia kuwa baada ya kuteka Kampala, kikosi chao kilipewa majukumu ya kwenda uwanja wa ndege ndogo wa mafunzo ya marubani wa kawaida katika Mji wa Soroti, kaskazini mwa Uganda na kumaliza operesheni. Mwaka 1979 walirejea nyumbani Tanzania.

***KESHO USIKOSE MOTO WA CHEO IGP NA MAZITO MATATU HATOSAHAU**

# CRDB Al Barakah yapata tuzo

**Na Mwandishi Wetu**

DIRISHA la kibenki la Kiislamu la Benki ya CRDB (CRDB Al Barakah) limetambuliwa kwa utendaji wake bora, likishinda tuzo ya 'Dirisha la Kibenki la Kiislamu Lililokuwa na Matumaini 2024' katika Tuzo za Fedha za Kiislamu za Kimataifa (GIFA).

Sherehe ya tuzo iliyofanyika Maldives, ilihudhuriwa na wawakilishi wa taasisi za kifedha kusherehekea ubora katika huduma za fedha za Kiislamu.

Heshima hiyo inafuatia mafanikio ya benki hiyo mwaka 2023 wakati ilipokiriwa kwa tuzo ya 'Dirisha la Kibenki la Kiislamu'.

Ukuaji mzuri na ubunifu wa CRDB Al Barakah katika kutoa huduma za kibenki zinazofuata sheria unazidi kuvutia wataalamu wa sekta na wateja, ikihakikisha sifa yake kama kiongozi anayeibuka katika sekta ya kibenki ya Kiislamu.

Wawakilishi wa Benki ya CRDB katika tukio hilo la heshima walikuwa Abdul Ally Mohamed, Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri wa Sheria (SAB), Rashid Rashid, Kiongozi wa Huduma za Kibenki za Kiislamu na Novati Mushi, Meneja wa Ushirikiano wa Kimkakati.

Tuzo hiyo inathibitisha dhamira thabiti ya benki hiyo katika kutoa huduma za kibenki za Kiislamu zinazofaa ambazo zinafuata kanuni za kifedha za Kiislamu, huku zikikidhi mahitaji ya kisasa ya wateja wake.

Mafanikio ya CRDB Al Barakah yanatokana na mambo kadhaa, ikiwamo ukuaji mkubwa ambao benki hiyo imeshuhudia mwaka uliopita.

Amana za kibenki za Kiislamu ziliongezeka kwa asilimia 317 kati ya robo ya kwanza ya mwaka 2023 na robo ya kwanza ya mwaka 2024.

Benki hiyo pia imeng'arishwa na ubunifu wake wa kiteknolojia katika kuwapa uzoefu wateja. Kwa kutoa bidhaa za kibenki za Kiislamu za kisasa kama vile Mkataba wa Ufadhili wa Murabaha kwa ajili ya mtaji wa kazi na ufadhili wa mali, pamoja na Mkataba wa Ufadhili wa Ijarah kusaidia hija ya Hajj na Umrah, CRDB Al Barakah imefanikiwa kupanua huduma zake na kukidhi mahitaji mbalimbali ya wateja wake.

Zaidi ya hayo, dhamira ya CRDB Al Barakah katika kujumuisha kifedha imekuwa na mchango mkubwa katika mafanikio yake ya kudumu. Kupitia huduma zake za kibenki za Kiislamu, CRDB inakuza uwezo wa kiuchumi huku ikifuata kanuni za kimaadili na kidini.

Umuhimu wa CRDB Al Barakah unazidi mipaka ya fedha za Kiislamu na kuingia katika uchumi mpana wa Tanzania. Benki hiyo imepeleka zaidi ya Sh. bilioni 90 katika mikopo na kuvutia Sh. bilioni 85 katika amana.


UCB CARING FOR FAMILY ECONOMY

## UCHUMI COMMERCIAL BANK LTD

### GHARAMA ZA HUDUMA KUFIKIA TAREHE 30.09.2024

| A | **DEPOSIT RATES** | **Descriptions** | **RATES(USD) - Products** | **RATES(TZS) - Products** |
|---|---|---|---|---|
| | Savings Account **(p.a)** | | | 1% |
| | Mavuno Account - Special Deposit Account (p.a) | | | 9% |
| | **Fixed Deposit** | | | |
| | 3 Months | | | 4% |
| | 6months | | | 5% |
| | 12Months | | | 6% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 50Mil | | | 6% to 7% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 100Mil | | | 8% to 9% |
| | Negotiable rates for Amount Exceeding 500Mil | | | 10% |
| B | **CHARGES AND FEES** | | | |
| | **ITEM/TRANSACTION** | | | **CHARGE/FEE** |
| 1 | **Current Accounts** | | | |
| | Minimum Opening balance - Company and individual | | 50.00 | 100,000.00 |
| | Minimum Operating Balance | | | - |
| | Monthly Statement enquiry | | 2.00 | TZS 1,500 per month and TZS 700 for extra page |
| | Monthly Ledger fee | | 5.00 | 15,000.00 |
| | Account closing charges | | 10.00 | 20,000.00 |
| | Sale of bankers cheque | | | 30,000.00 |
| | Cancelation of bankers cheque | | | 30,000.00 |
| | Cheque book per leaf | | 0.18 | 400.00 |
| | Stop payment order | | 10.00 | 30,000 reported lost/stolen cheque book/leaf (per notice) |
| | Standing order within the bank per entry | | 2.00 | 2,000.00 |
| | Standing order to other banks per entry | | 20.00 | 15,000.00 |
| | Confirmation of Balance and Audit statement | | 25.00 | 50,000.00 |
| | Salary processing fee per entry | | N/A | 2,000.00 |
| | Upaid cheque (RD) | | 40 | 40,000.00 |
| | Montly fees - Parishes Account | | N/A | 5,000.00 |
| | - Other Current Account | | N/A | 15,000.00 |
| | Quartely fees - Other Current account | | 5 | 2,000.00 |
| | Current Accounts - Individual withdrawal over counter | | 5 | 2,000.00 |
| | Current Accounts - Individual monthly fees | | 5 | 5,000.00 |
| | Current Accounts - SACCOS withdrawal over counter | | | 2,000.00 |
| | Deposit fee | | | free |
| | Withdrawal on current account using cheque | | | |
| | | 1 - 399,999 | | 1,500.00 |
| | | 400,000 - 4,999,999 | | 1,800.00 |
| | | 5,000,0000 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 and above | | 0.05% |
| | Withdrawal on current account without cheque | Any Amount | | 5,000.00 |
| 2 | **Savings Accounts** | | | |
| | Minimum Operating Balance | Mavuno Saving Account | | 5,000.00 |
| | | Personal Saving | 10 | 10,000.00 |
| | | Other Savings Products | | 10,000.00 |
| | Account closure | | 10 | 20,000.00 |
| | Dormant account reactivation | | | free |
| | Withdrawal fee over the counter- Savings Products | | 1% of the withdraw amount | |
| | | 1 - 399,999 | | 1,500.00 |
| | | 400,000 - 4,999,999 | | 1,800.00 |
| | | 5,000,0000 - 9,999,999 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 and above | | 0.05% |
| | Account maintenance fee - Monthly - Saving products | | | 1,500.00 |
| | - Quartely - Saving products | | | 1,600.00 |
| | Bulk Cash deposit | | | free |
| | New ATM card issuance | N/A | | 10,000.00 |
| | ATM card renewal or replacement | N/A | | 15,000.00 |
| | ATM withdrawal fee | 1,000 - 99,999 | | 1,500.00 |
| | | 100,000 - 400,000 | | 1,700.00 |
| | PIN Reset ATM | | | 5,000.00 |
| 3 | **Electronic Banking** | | | |
| | SWIFT/TISS transfer | 1 - 10,000,000 | | 2,000.00 |
| | | 10,000,000 - 50,000,000 | | 5,000.00 |
| | | 50,000,000 and above | | 10,000.00 |
| | Mobile banking balance enquiry | | | 300.00 |
| | Transfer from bank account to mobile - As per TIPS schedule below | | | |
| | Mobile - PIN reset | | | 2,000.00 |
| | **Other Charges** | | | |
| | Cheque clearing fee (Outward Cheques) | | | 1,000.00 |
| | EFT | | | 2,000.00 |
| | Search fees (including vouchers) | one Month | | Free |
| | | Two(2) to six(6) month | 10 | 20,000 |
| | | Above six(6) month | 25 | 50,000 |
| | | CCTV footage Maximamu of 3 months | Tzs equivalent | 30,000 |
| | | | | |
| | Uncollected cheque book (after notification) | | | TZS 2,000 per month |
| | Coins deposit | Percentage of deposit amount for non parish | | 3% |
| | Brela Search Fees | Company Limited | | TZS 25,000 |
| | | Trade name | | TZS 7,000 |
| 4 | **Internet Banking** | | | |
| | 24/7 Transfer UCB to UCB | | | Free |
| | 24/7 Transfer (Other Banks) | | | AS PER TIPS AND TISS SCHEDULE |
| | 24/7 Fund transfer (Bank to Mobile) - as per TIPS schedule below | | | |
| | 24/7 Airtime processing | | | free |
| | 24/7 Government payment | | | free |
| | 24/7 Other payments (utility) | DSTV, Star Times, AZAM, Subsciption services, bettings, Air tickets etc. | | 1,500.00 |
| | Balance inquiry | | | Free |
| | Monthly fee per retail user | | | 1,500.00 |
| | Monthly fee for corporate user | | | 2,500.00 |
| | Retail & Corporate subsricption | | | Free |
| | Bank statement self download | | | 500.00 |
| | Cheque book request 100 leaves | | | 47,200.00 |
| | Cheque book request 50 leaves | | | 23,600.00 |
| | PIN Regeneration | | | Free |
| | Salary processing | | | 500.00 |
| | Standing Order Instructions | | | 2,000.00 |
| | TIPS | 1 - 50,000 | N/A | 500.00 |
| | | 50,000 - 500,000 | N/A | 1,000.00 |
| | | 500,000 - 5,000,000 | N/A | 1,500.00 |
| | | 5,000,000 - 20,000,000 | N/A | 2,000.00 |
| 5 | **Agency Banking** | | | |
| | Agent Cash withdraw charges | 1,000-29,999 | N/A | 1,500.00 |
| | | 30,000-49,999 | N/A | 1,500.00 |
| | | 50,000-99,999 | N/A | 1,500.00 |
| | | 100,000-299,999 | N/A | 1,600.00 |
| | | 300,000-499,999 | N/A | 3,200.00 |
| | | 500,000-999,999 | N/A | 3,250.00 |
| | | 1,000,000-1,999,999 | N/A | 4,450.00 |
| | | 2,000,000-2,999,999 | N/A | 6,550.00 |
| | | 3,000,000-3,999,999 | N/A | 7,650.00 |
| | | 4,000,000-4,999,999 | N/A | 8,750.00 |
| | | 5,000,000-5,999,999 | N/A | 9,850.00 |
| | Agent cash deposit | | | Free |
| | Agency Banking - Balance enquary | | | 500.00 |
| | | | | |

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaorudisha nyuma maendeleo wanapaswa kuadhibiwa

**TUKIO** lililotokea katika Kata ya Tembela, jijini Mbeya la watu wasiojulikana kubomoa madarasa mapya yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi linarudisha nyuma maendeleo.

Wananchi wamejitolea kutumia nguvu zao kujenga madarasa hayo ili kupunguza uhaba wa vyumba vya kusomea, lakini watu wachache wasiopenda maendeleo wameamua kuyabomoa.

Tukio hilo limezua taharuki kwa sababu limefanyika usiku, ikionesha kuwa watu hao walikuwa na nia ovu ya kudhoofisha nguvu za wananchi hao.

Kwa mujibu wa mwananchi mmoja wa eneo hilo, wananchi kwa kuchangishana fedha waliamua kujenga madarasa hayo na hakukuwa na mgogoro wowote wa ardhi.

Aidha, wananchi hao waliamua kuchangishana Sh. 12,000 kila mmoja ambazo kwa sehemu kubwa zinatokana na biashara ya mazao wanayolima.

"Kitendo hichi kimetushtusha sana, sisi hatuna vyanzo vikubwa vya mapato zaidi ya kilimo ambacho ni cha msimu, tumeshindwa kuelewa hawa watu wana nia gani kwa sababu hapa hapana mgogoro wowote wa ardhi kwamba useme ndio unaosababisha," anasema mmoja wa wananchi hao.

Ukitafakari matukio kama hayo yanafanywa na watu wasio na nia njema na wanaopenda kuona kila mara kukitokea migogoro na vurugu ili kuharibu amani iliyopo.

Watu waliofanya tukio hilo wana nia ovu ya kudhoofisha harakati za wananchi wapenda maendeleo wanaopenda kuona nchi yao ikisonga mbele katika sekta ya elimu.

Kama wakulima wameamua kuchanga sehemu ya mapato yao ili yaweze kujenga madarasa ya kusomea watoto wao, na pengine hata hao walioshiriki kuyabomoa kuna watoto wao ambao wangesoma kwenye madarasa hayo, lakini wameamua kufanya uovu huo bila kufikiri siku za usoni yatakuja kusaidia vizazi vyao.

Matukio yenye kuashiria uvunjifu wa amani yanapotokea katika eneo moja kila wakati, yanafanya watu wajiulize kulikoni, hata kama kuna kitu hakiko sawa njia nzuri ni kukaa pamoja na kufikia mwafaka, lakini si njia ya kufanya uharibifu wa miundombinu ambayo itakuja kusaidia vizazi vya sasa na vya baadaye.

Kwa mujibu wa kiongozi mmoja wa eneo hilo, awali lilianza kubomolewa jengo la mtaa wa Tembela na baadaye likabomolewa jengo la mtaa wa Relini na kwamba majengo hayo yalibomolewa kwa siku tofauti.

Ilidaiwa kuwa mwanzo wananchi walifikiri jengo walilolikuta limebomoka, walifikiri limejengwa chini ya kiwango, lakini lilivyobomolewa la pili wakajua kuna watu wenye nia ovu walioshiriki kufanya uharibifu huo.

Wanaofanya vitendo hivyo vya uharibifu wanapaswa wajitafakari badala ya kufanya uamuzi ambao hauna tija na kudidimiza kasi ya wananchi wanaopenda maendeleo ya nchi yao.

Ndio maana kuna haja ya watu kwenda kupima afya ya akili ili kujitambua kama wako sawa. Kwa sababu mwenye afya ya akili iliyo sawa hawezi kuchukua uamuzi huo usio na tija.


Serikali inafanya juhudi kuhakikisha shule zinakuwa na madarasa ya kutosha ili kila mtoto anayekwenda kupata elimu, anaipata katika mazingira yaliyo bora.

Na kwa kuitikia wito huo wa serikali, wananchi wameamua kujitolewa nguvu zao kuanza ujenzi wa madarasa kwenye maeneo ambayo bado hayajafikiwa na bajeti, ili yatakapofikiwa bajeti imalizie mambo mengine.

Lakini, waliofanya uharibifu huo ni lazima wasakwe na kuchukuliwa hatua.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com



Na Jane Mathias

## Muungwana Lazima Nilonge

# Baba Nyerere hata sasa tunathamini uliotuachia

**TANZANIA** imeadhimisha kumbukizi ya miaka 25 ya kifo cha mwasisi wake, Mwalimu Julius Nyerere kilichotokea Oktoba 14, 1997 nchini Uingereza , wakati akitibiwa saratani ya damu.

Kumbukizi hizo zilizofanyika jana mkoani Mwanza zikiambatana na kuzima Mwenge wa Uhuru katika Uwanja wa CCM Kirumba, mgeni rasmi akiwa Rais Samia Suluhu Hassan.

Kwa ujumla taifa linamkumbuka Nyerere kwa kuwa mwasisi wake tangu kupigania uhuru kutoka kwa wakoloni wa Uingereza, hadi kuweka misingi ya kujitegemeza kiuchumi, kisiasa, kiuongozi na mifumo muhimu ya maendeleo inayoonekana leo.

Mifumo hiyo ni kama viwanda, umeme, maji, barabara na miundombinu ya reli, madaraja, majengo ya umma na hata taasisi kuanzia vyuo vikuu, sheria na bunge. Kuna mambo mengi mazuri aliyolifanyia taifa na baadhi ya nchi za Afrika kupata uhuru kutoka kwa wakoloni, jamii inapaswa kuyaendeleza kwa manufaa ya vizazi vya sasa na vijavyo.

Yapo ambayo yanapaswa kumuenzi Mwalimu ikiwa ni pamoja na kuhifadhi mazingira. Itakumbukwa wakati wa uhai wake alikuwa mstari wa mbele kupiga vita uharibifu wa mazingira ili kuepusha nchi na jangwa, ukame lakini ukiwezesha kupata mvua za kutosha zinazoleta maji ya kunywa na mifugo na kuendesha kilimo cha mazao ya chakula na biashara.

Kwa upande wa siasa, baadhi ya viongozi wanatakiwa kumuenzi kwa kujenga utamaduni wa kukubali kukosolewa pale ambapo mambo yanakwenda ndivyo sivyo. Wanatakiwa kuendeleza umoja na kuacha ukabila, umimi, kugeuka miungu watu kwenye uongozi na kama alivyofanya, kung'atuka badala ya kuendelea kung'angania kubaki madarakani ili kujilindia heshima katika jamii.

Viongozi wanatakiwa falsafa ya kujitegemea ili Tanzania ijenge uchumi imara kwa kutumia rasilimali za ndani kwenye kilimo, madini, mafuta na gesi ili kutimiza kauli mbiu ya kujitegemea ambayo alikuwa akiitumia mara kwa mara kama njia ya kuwahimiza viongozi na wananchi ili kuondokana na umaskini.

> **Rais huyo wa kwanza wa Tanzania, kwa kutumia falsafa yake hiyo ya kilimo, aliwaagiza viongozi wa serikali na wananchi kushiriki, shabaha yake kuu ikiwa ni kuinua uchumi wa vijijini na kuboresha maisha ya wananchi.**

Nyerere alitilia mkazo kilimo kwa sababu alibaini kuwa ni njia pekee kwa wananchi wengi ambao ni wakulima ya kuboresha maisha yao na taifa kuondokana na njaa kwa kuzalisha chakula cha kutosha na ziada kwa ajili ya biashara.

Rais huyo wa kwanza wa Tanzania, kwa kutumia falsafa yake hiyo ya kilimo, aliwaagiza viongozi wa serikali na wananchi kushiriki, shabaha yake kuu ikiwa ni kuinua uchumi wa vijijini na kuboresha maisha ya wananchi.

Katika maeneo hayo, aliwasisitiza wananchi kuishi na kufanya kazi kwa kushirikiana pamoja vijijini ili kuongeza uzalishaji katika kilimo kwa kushirikiana kwa rasilimali za ardhi, zana na nguvu kazi.

Vilevile alianzisha vyama vya ushirika na ya kuwaunganisha wakulima ili kuwainua wakulima wadogo na kuimarisha uwezo wao kwa faida, kupata pembejeo kwa urahisi na kuinua hali zao kwenye mauzo ya kahawa, pamba, korosho na chai. Kuhusu elimu, tunapaswa kumuenzi kwa kutilia mkazo kuwa kila mtoto awe wa maskini au tajiri anapata elimu sawa na mwingine kwa kuwa ni haki ya kila mmoja kwa manufaa yake na taifa zima.

Wiki hii ni wakati wakumkumbuka Mwalimu na mambo mengi ambayo alikuwa mstari wa mbele kuyatetea au kuyapiga vita kama rushwa na vitendo hivyo bado vinalalamikiwa kukithiri katika taasisi za serikali, hivyo kuwa chanzo cha kuwanyonya wananchi wanapohitaji kupata huduma.

Vitendo hivyo, vimekuwa vikilalamikiwa na wananchi wanyonge ambao wamekata tamaa kwa kukosa huduma muhimu na maisha yao kuzidi kuwa duni. Kwa kumuenzi Nyerere wananchi kataeni kutoa rushwa na kuwafichua wanaojihusisha nayo kwa manufaa yetu na vizazi vijavyo.

## HABARI KITAIFA



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, akionesha sehemu ya samaki waliovunwa kwenye vizimba vya ufugaji samaki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# BBT uvuvi yaanza kulipa vijana wafugaji

**Na Mwandishi Wetu**

MAONO ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ya kuwezesha vijana kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyobora (BBT) yameanza kuzaa matunda baada ya kuwezeshwa kufuga samaki kwenye vizimba jijini Mwanza na kuanza kuvuna.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema hayo aliposhiriki awamu ya kwanza ya uvunaji samaki aina ya sato uliofanywa na Kikundi cha Vijana cha TWIHAME kinachofanya shughuli zake za ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika eneo la Kisoko, Kata ya Luchelele, wilayani Nyamagana jijini Mwanza, mwishoni mwa wiki.

Akizungumza baada ya kushiriki uvunaji, Waziri Ulega alimshukuru Rais Dk. Samia kwa kutoa Sh. bilioni 2.2 na kuviwezesha vikundi 11 vya vijana kufanya ufugaji wa samaki katika eneo la Kisoko na kuwekeza vizimba zaidi ya 100 katika eneo hilo.

"Leo katika kizimba hiki kimoja tu ambacho watavuna samaki takriban 4,000, vijana hawa watapata kiasi cha shilingi zaidi ya milioni 30, inaleta matumaini makubwa sana, na mwitikio wa uwekezaji katika Ziwa Victoria kupitia vizimba ni mkubwa sana, mwitikio huo utasaidia kupunguza masuala ya uvuvi haramu kwa sababu wavuvi wanakwenda kuwa na kazi mbadala," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa vizimba, ambaye pia ni Katibu wa wanufaika, Wilaya ya Nyamagana, Omary Mangu, alimshukuru Rais Dk. Samia kwa kuwawezesha mkopo ambao hauna riba ili waweze kufanya shughuli za kufuga samaki na matunda ya mkopo huo wameanza kuyaona.

Septemba 25, 2024, Vijana wa Kikundi kingine kinachojulikana kwa jina la Nguvu Kazi walianza kuvuna tani 13.37 kutoka katika vizimba sita na baada ya kuwauza walifanikiwa kupata zaidi ya Sh. milioni 100.

Januari 30, mwaka huu, akiwa jijini Mwanza, Rais Samia alizindua mradi wa vizimba 222 na boti 160 kwa ajili ya kuwakopesha wavuvi nchi nzima ili waweze kufanya shughuli zao kwa tija na kuboresha kipato chao.

# Dar kinara matumizi nishati chafu kupikia

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila amesema mkoa wake ni kinara wa matumizi ya nishati chafu kutokana na kuwa na idadi kubwa ya watu.

Amesema Mkoa wa Dar es Salaam unaongoza kwa matumizi ya kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia na jitihada za haraka zinahitajika ili kunusuru tatizo hilo.

Alisema hayo jana katika viwanja vya Biafra, Kinondoni mkoani Dar es Salaam wakati akipokea msaada wa mitungi ya gesi 1,000 kutoka kampuni ya Puma Energy Tanzania kwa ajili ya kuwapatia mama na baba lishe.

Chalamila alisema msaada huo umekuja wakati sahihi kwani dhamira ya Rais Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha wananchi wote ifikapo mwaka 2030 wanatumia nishati safi katika kupika.

Alisema kupika kwa gesi ni nafuu kulinganisha na kuni au mkaa ambao hata madaktari wameshabainisha kuwa na madhara makubwa kiafya ikiwamo magonjwa ya saratani na hewa, macho.

"Dar es Salaam ndiyo mkoa unaotumia nishati chafu kutokana na wingi wa watu wanaotumia kuni na mkaa kwa ajili ya kupikia, hivyo uamuzi wa Puma Energy Tanzania unakwenda kumaliza au kupunguza matumizi ya nishati chafu katika mkoa wangu na Tanzania kwa ujumla," alisema.

Akigusia faida za matumizi ya nishati safi, Chalamila alisema inaokoa muda mwingi unaotumika kupika kwa kuni na mkaa, kuokoa gharama pamoja na kuepuka madhara ya kiafya.

Mkurugenzi Mkuu wa Puma Energy Tanzania, Fatma Abdallah, alisema lengo lao ni kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika kampeni ya matumizi ya nishati safi ya kupikia na ndiyo sababu wametoa msaada wa mitungi hiyo kwa mama na baba lishe.

Alisema mkoani Dar es Salaam kuna shughuli nyingi ikiwemo biashara ya chakula kinachoandaliwa kwa wingi kutoka kwa mama na baba lishe ambao wanakumbana na changamoto nyingi kama vile upatikanaji wa nishati ya kupikia hususani nishati safi na salama.

Alisema wanaelewa dhamira ya serikali ambayo imekuwa na mpango kazi kwa miaka kadhaa wa kuelimisha na kueneza matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa wananchi.

Alisema jitihada hizo zimeonyesha katika mikutano ya ndani na nje ya nchi ambayo Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akishiriki kuhakikisha upatikanaji na matumizi ya nishati safi yanaimarika.


## IN LOVING MEMORY
### of Gosbert Stanslaus Mutagaywa



*Today, October 15th, 2024 marks 4 years since you left us. Years have passed, and now your presence is difficult to find. But the memories of our time together are still fresh in our minds. We think about you always, and we talk about you still. You have never been forgotten, and you never will. Your darling wife- Irene, your lovely daughter- Evelyn, Sister-Rosemary, sisters-in-law, brothers-in-law, other relatives, colleagues, friends, and our neighbors miss you every day and will forever love you.*

*Gone from our sight, but never from our hearts.*

***Revelation 21:4***

*He will wipe every tear from their eyes,and death shall be no more, neither shall there be mourning, nor crying, nor pain anymore, for the former things have passed away.*

# Kaya 300 zaamriwa kuhama kijiji Kilindi

**Na Hamida Kamchalla,** KILINDI

KAYA 300 za jamii ya wakulima wa Kijiji cha Kinkwembe wilayani hapa Mkoa wa Tanga, zimemwomba Rais Samia Suluhu Hassan kutengua amri ya kuondolewa kwa maeneo yao kupisha uhifadhi wanyamapori.

Wakazi hao wametoa ombi hilo baada ya kupewa siku 14 kuondoka katika kijiji hicho kwa madai kuwa nyumba na mashamba yao yao vipo ndani ya ushoroba wa wanyamaori.

Wakizungumza na Nipashe, walidai hawajui hatima yao na familia zao, baada ya Mkuu wa Wilaya ya Kilindi, Hashim Mgandilwa kuamuru waondoke na kukataa kusikiliza ombi lao.

Mmoja wa wakazi hao, Mathias Ernest, alidai kinachowaumiza ni kuamriwa waondoke huku wenzao wa jamii ya wafugaji wa Kimasai wakiachwa waendelee maeneo ya kijiji hicho bila kubughudhiwa.

"Tunaomba Mheshimiwa Rais atusikilize kilio chetu, tayari tumefungua tawi, tumejiandikisha kuwa wanachama halali wa CCM tuko zaidi ya 200 na usajili wetu umekamilika," alidai na kuongeza kuwa:

"Tunategemea kupiga kura, tunaamriwa tuondoke, hatujui tunakwenda kupiga kura wala kuishi wapi, familia zinateseka."

Halima Mmbelwa, alidai kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15 amekuwa akifanya shughuli zake za kilimo na kujipatia kipato cha kuendesha maisha yao katika eneo hilo.

Mwinjuma Sufian alidai kuwa: "Kutokana na amri hiyo hawataweza kushiriki kwenye upigaji wa kura baada ya kukosa msaada kwenye chama wanachokifuata."

Wiki iliyopita, Mgandilwa akiwa kwenye kijiji hicho, alitoa siku 14 kwa wakulima hao kuhama kwa kuwa eneo hilo ni ushoroba wa wanyamapori.

"Nawaomba wananchi wote ambao mmejenga, hapa sio maeneo ya makazi, tayari yameshapangwa matumizi yake.

...Mmeletwa Kinkwembe rudini kijijini wawatafutie maeneo na mlioletwa kutoka Lengusero nendeni kule wawatafutie maeneo mengine bado maeneo ya kuishi tunayo mengi sana," alisisitiza mkuu huyo wa wilaya.



Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu, akipewa maelekezo kuhusu ulimaji bora wa miwa, alipotembelea mashamba ya miwa ya kiwanda cha Kilombero baada ya kuzindua Siku ya Wakulima wa Miwa Bonde la Kilombero wilayani Kilombero, mkoani Morogoro juzi. Mkuu wa Wilaya ya Kilombero, Dustan Kyobya na kulia ni Mkuu wa Wilaya ya Kilosa, Shaka Hamdu Shaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Madaktari JKCI wapiga kambi Arusha

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

TAASISI ya Moyo ya (JKCI), imeanza kambi ya siku nne kwa ajili ya kupima afya kwa wakazi mkoani hapa na jirani na kutoa matibabu kwa watakaobainika kuwa na maradhi ya moyo kuanzia leo.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, akizungumza jijini hapa juzi, alisema wameandaa kambi hiyo kwa kushirikiana na Arusha Lutheran Medical Center.

Dk. Kisenge alisema wameshirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Arusha, kuandaa kambi hiyo kuanzia Oktoba 15 mpaka 18 mwaka huu katika Viwanja vya Arusha Lutheran Medical Center.

Aliwaomba wakazi hao kujitokeza kwa wingi kupima afya zao na watakaogundulika kuwa na matatizo ya moyo watapatiwa matibabu na wengine kupewa rufani kwenda jijini Dar es Salaam, Taasisi ya Moyo Jakaya Kikwete (JKCI).

Alisema kwenye kambi hiyo wataalamu wa lishe watakuwapo kutoa elimu ya kula vyakula ili kuepukana na magonjwa yasiyo ya kuambukiza yakiwamo ya moyo.

"Watu wajitokeze watumie fursa hii kwasababu watakaobainika kuwa na matatizo ya moyo watapatiwa matibabu hapo hapo au kupewa rufani kwenda JKCI Dar es Salaam," alisema.

Alisema jamii inapaswa kujenga utamaduni wa kupima afya ya moyo mara kwa mara kwa kuwa baadhi wanaishi na maradhi hayo bila kujua, na kama wangegundua wangepata matibabu mapema.

Aliwataka wananchi kuzingatia ushauri wa wataalamu kuhusu lishe bora ili kuepuka maradhi.

Kwa mujibu wa Dk. Kijenge, JKCI imeendelea kujiimarisha kwa kuwa na vifaa tiba vya teknolojia ya kisasa na wataalamu bobezi wa moyo hali ambayo imepunguza utegemezi wa kupeleka wagonjwa wa moyo kwa matibabu nje ya nchi kwa zaidi ya asilimia 90.

# EPZA yasisitiza umuhimu elimu kwa wawekezaji

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Uwekezaji kwa Mauzo Nje ya Nchi (EPZA) imesisitiza umuhimu wa kutoa elimu na taarifa ya fursa za uwekezaji zilizoko nchini ili wawekezaji wa ndani na nje kufanya uamuzi sahihi wa uwekezaji.

Akizungumza katika maonesho ya saba ya kitaifa ya teknolojia ya madini yaliyomalizika hivi karibuni mkoani Geita, Ofisa wa Uhamasishaji Uwekezaji wa EPZA, Blandina Mwasamwene, alisema Mamlaka hiyo inajikita kutoa elimu ya fursa zilizoko katika sekta mbalimbali kama vile madini, uzalishaji na kilimo.

"Kutoa elimu ya uwekezaji ni muhimu kwa kuwapa uwezo raia wa Tanzania na wawekezaji wa kigeni kufanya maamuzi sahihi katika soko lenye ushindani wa hali ya juu," alisema.

Kwa kutoa maarifa muhimu kuhusu michakato ya uwekezaji, mifumo ya kanuni, na mwenendo wa soko, EPZA inawasaidia watu kuelewa fursa na changamoto za mazingira ya biashara.

Uelewa huu unajenga imani, unahamasisha ushiriki katika uchumi na hatimaye unachangia kuanzisha miradi ya uwekezaji yenye mafanikio ambayo inaweza kuchangia maendeleo ya taifa.

Wakati wawekezaji wanakuwa na maarifa ya kutosha, wana uwezo mkubwa wa kubaini na kushika fursa zenye faida, jambo ambalo linaweza kuleta uundaji wa ajira na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi. Athari hii inafaida sio tu wawekezaji binafsi bali pia inaimarisha uchumi mpana, ikisaidia malengo ya ukuaji na maendeleo endelevu ya Tanzania.

Alisema kuhamasisha uwekezaji katika sekta zinazohusiana na madini, EPZA inatarajia kuimarisha mnyororo wa thamani, kuanzia uchimbaji hadi usindikaji, jambo ambalo si tu linaunda ajira bali pia linaimarisha maendeleo ya teknolojia.

Aidha, alisema EPZA inaendeleza juhudi za serikali za kutoa elimu ya uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na wa kigeni.

"EPZA ina wajibu wa kuwezesha upatikanaji wa leseni kwa wawekezaji, ili kuwapa uwezo wa kupata maeneo maalum ya kujenga viwanda, ikiwa na masharti ya kuuza asilimia 20 ya bidhaa zao ndani ya nchi na asilimia 80 kimataifa."

Mamlaka hiyo pia imeweka maeneo ya uwekezaji wa viwanda katika mikoa na wilaya mbalimbali, ikiwa ni pamoja na maeneo yaliyoendelezwa kwa miundombinu inayowaruhusu wawekezaji kuanzisha viwanda haraka.

Baadhi ya maeneo haya ya kimkakati ni pamoja na Bagamoyo katika mkoa wa Pwani, Manyara, Mtwara na Tanga, pamoja na maeneo mengine nchini, yote yakiwa tayari kwa miradi mipya ya viwanda.

MAKALA MAALUM

# MALECELA, 1934 -2024 NINA YAFUATAYO:

## • Watu saba duniani waliomtoa Mandela jela • Hifadhi Saanane, pundamilia nikatoa Rudolf Kenya • Ubunifu mfumo wa upigaji kura uliopo sasa • Kuanzisha ubalozi Marekani, pia vyama vingi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

***GAZETI la jana lilikuwa na sehemu ya kwanza ya mazungumzo maalum ya Nipashe na Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela, nyumbani kwake jijini Dodoma, Alhamisi iliyopita namna alivyohusiana na Rais wa Kwanza Hayati Julius Nyerere. Endelea na sehemu ya pili, inayohusu maisha yake na utumishi wa umma.***

“MWANZA kuna kitu kimoja nilikianzisha, hadi sasa kipo na nasema kwa unyenyekevu mkubwa mimi ndiye niliyeanzisha Hifadhi ya Kisiwa cha Saanane, nikiwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, wakati huo ukiitwa East Lake Province,” ni sehemu ya nukuu za simulizi kuhusu maisha ya Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela, alipozungumza na Nipashe.

Anasimulia kwamba hifadhi hiyo ilianzishwa kama Bustani ya Kwanza ya Wanyama nchini Tanzania, mwaka 1964 na ikawa hifadhi kamili mwaka 2013, akinena lengo na sababu za kuanzisha, ikaitwa Saanane, ana maelezo:

“Niliporudi kutoka Chuo cha Cambrige (Chuo Kikuu - England) niliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza. Lakini, wakati huo ulikuwa unaitwa East Lake Province, ambayo sasa hivi imegawanywa na kupata mikoa mingine ya Geita, Shinyanga, Mara na Simiyu.”

Anasema kisiwa hicho kipo Magharibi mwa Bandari ya Mwanza na kilikuwa kinavutia, watu walipokuwa wanaingia na kutoka mkoani humo.

“Pale Mwanza Port (Bandari Mwanza) upande wa Magharibi ukiangalia mbele, kuna ‘kakisiwa’ kazuri sana. Sasa kale mimi nilitaka nikafanye kama bustani, kwa hiyo nikapeleka pale simba, tembo, pundambilia.

“Na pundamilia niliyopeleka pale walikuwa ni ‘special’ (maalum), sio wenye mistari kama ilivyozoeleka, wao walikuwa na mistari iliyonyooka niliwatoa Ziwa Rudolf (Kenya),” anasema.

Anabainisha kuwa hadi sasa, moja ya kitu anachojivunia nacho ni kuwapo hifadhi hiyo, kivutio kwa wananchi wanaofika Mwanza.

“Ninajivunia sana, kwa sababu hadi leo watu wanaenda kutalii, na jina la Saanane lilitokana na jina la mzee mmoja pale kwenye kisiwa aliitwa Saanane Chawandi. Alikuwa akiishi hapo, nikaona ni busara hiyo bustani ibebe jina hilo,” anasema.

Anasema ni kisiwa kilichoko katika mandhari ya kupendeza na inavutia, akaona liwe eneo la kupumzikia wananchi wanaofanya safari mbalimbali, hasa treni.

“Kwanini nilifanya hivyo? kwasababu treni linalotoka Dar es Salaam ilikuwa inafika Mwanza saa mbili asubuhi na treni inayotoka Mwanza kuja Dar es Salaam.

“Lilikuwa linaondoka saa tisa mchana, sasa nikafanya kisiwa kile kiwe ni kisiwa ambacho badala ya watu kukaa stesheni muda mrefu, wanakwenda kwenye kisiwa wanazunguka wanapanda treni wanaendelea na safari zao,” anasimulia Mzee Malecela.

Anafafanua kuwa mkoa huo aliyouongoza, ulikuwa unaheshimika na ulikuwa ukichangia Pato la Taifa kwa asilimia 40. Malecela ana maelezo: “Mkoa wa Mwanza ulikuwa unachangia kiasi hicho kwa sababu tulikuwa na almasi Mwadui, dhahabu Geita, pamba, kuna wakati tulitoa pamba nyingi sana kuliko Uganda.

“Tulikuwa wazalishaji wakubwa wa pamba kwa Afrika Mashariki, kwa hiyo utaona mkoa niliokwenda kuwa Mkuu wa Mkoa ulikuwa ni mkoa wenye neema.”

“Nakumbuka kulikuwa na chama cha ushirika kiliitwa Victoria. Kilikuwa chama chenye nguvu kwa Afrika Mashariki nilipokwenda baada ya muda kidogo tuliweza kuingiza matrekta 40.

“Nakukumbuka wakati huo, bado kijana tunazunguka na matrekta mtaani, ilikuwa ni kitu cha kutisha sana,” anatamka na kuendeleza simulizi:

“Nashukuru kwa kweli katika watu ambao hawahitaji kuambiwa ‘fanya kazi kwa bidii’ ni msukuma! Ni watu wanaojituma kwa hiyo uzalishaji wa pamba ulikwenda juu sana na mazao mengine.”

### HISTORIA YAKE

Anasema, alisoma katika Shule ya Msingi Kijiji cha Mvumi na baadaye kujiunga na elimu ya sekondari katika Shule ya Alliance na kumalizia Minaki.

“Nilipata ufadhili wa kwenda Chuo cha Bombay, India, kwa hiyo, mwaka 1955 niliende kusoma na kumaliza mwaka 1959. Niliporudi nilikaa kama raia na baada ya hapo 1960 niliajiriwa na serikali ya kikoloni wakati huo, nikapelekwa Tukuyu kuwa Msaidizi wa Kwanza wa Mkuu wa Wilaya,” anasema.

Anaeleza kuwa alipotoka Tukuyu, alihamishiwa Mbeya na baadaye Wilaya ya Mbozi, alikotumikia nafasi hiyo na eneo hilo kulikuwapo Wazungu wanalima kahawa.

“Nilipata nafasi ya kwenda kusoma Ulaya Chuo cha Cambridge (Chuo Kikuu - Ungland). Kina heshima yake, nadhani hivi karibuni kilifikisha miaka 800.

Anasimulia kuwa Tanganyika ilipopata Uhuru ikaingizwa kwenye umoja huo na Balozi wa Kwanza alikuwa anaitwa Dk. Feda Kihaluzi na yeye akawa ‘Councillor’ (balozi) chini yake.

“Mwaka 1963 nikarudi nyumbani, nikapelekwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza. Wakati huo kila tulipokuwa tunakwenda unachukua nafasi iliyokuwa ya mzungu.

“Sasa mwenzangu aliyenitangulia alikuwa anaitwa Richard Wambura, alichukua kutoka kwa mzungu, nilikaa Mwanza hadi mwisho wa mwaka 1964 nikateuliwa kuwa Balozi wa Tanzania Umoja wa Mataifa,” anasema.

### TUME WATU SABA

Anasimulia, alipokuwa Balozi kwenye Umoja wa Nchi za Afrika Addis Ababa (OAU), aliteuliwa kwenye tume ya watu saba maarufu duniani na Jumuiya ya Madola, ili kwenda kusuluhisha tofauti kati ya Wazungu na Waafrika nchini Afrika Kusini.

“Tume ile tulipeleka mapendekezo yetu na ndio baadae, yakaleta kuachiliwa kwa (Nelson) Mandela gerezani. Tume yetu ya watu saba tulikuwa ndio watu wa kwanza wa kimataifa kuonana na Mandela akiwa jela,” anasema.

Anaongeza: “Tulileta ripoti yetu kwenye Jumuiya ya Madola na mimi ningependa kuamini kwamba, kutokana na ripoti yetu, watu wa Afrika Kusini walimuachia Mandela.”

Pia, anabainisha kuwa baada ya kazi ya tume hiyo, aliporudi nchini aliteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa na mwisho wa mwaka 1988, aliteuliwa kuwa Balozi wa Tanzania nchini Uingereza.

“Baada ya kutoka Uingereza mwaka 1990, nikateuliwa Waziri Mkuu na Makamu wa kwanza wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hadi 1994,” anaeleza.

### ALIVYOANZA SIASA

Anasema alianza kujishughulisha na siasa akiwa mwanafunzi na kwamba wakati huo India ilikuwa imepata Uhuru wake Mwaka 1949.

“India iliahidi kuwasaidia vijana wa Kiafrika kwenda kusoma kule, ili kuja kuharakisha uhuru wa Afrika. Sasa, mimi nilikuwa mmojawapo wa walipata ufadhili, nikasoma.

“Na kule usingeweza kukaa kwa njia yoyote bila kuwa mwanasiasa, kwa sababu wakati huo na bara la Afrika lilikuwa linachemka, mtakumbuka wakati ule vijana wa Soweto (Afrika Kusini- Juni 16, 1976) wanaandamana, mimi ndio wakati huo nilizaliwa kisiasa,” anasimulia Mzee Malecela.

Anafafanua kuwa, suala la siasa kwake halikuwa zaidi la utashi wa kuingia katika chama, bali ni kujijenga kifikra kuwa muhimu kujitawala.

“Wakati huo ulikuwa mgumu, walikuwa (mataifa makubwa) wanasema nyie kweli mtajitawala kwanza, hamna hiki hamna hiki!

“Tukasema, hapana hata kama hatuna, lakini tunachotaka kama Muingereza anaweza kukaa akatuamrisha, kwanini tusikae tujiamrishe wenyewe?” anaeleza.

‘Na mtuache tujiamrishe wenyewe kama kukosea basi mje mtukosoe, kwa hiyo siasa haikuwa kama kuingia kwenye chama kama siku hizi,” anasema.

### UJIO VYAMA VINGI

Malecela anasimulia kumbukizi yake, akiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, kwamba vilivyojitokeza wakati wake na hatosahau, ni ujio wa mfumo wa vyama vingi.

“Mwaka 1991 serikali iliamua kuunda Tume ya Nyalali (Jaji Mkuu Francis Nyalali) na wakati huo ndio ulikuwa wakati Waafrika wanalia hata chama kimoja. Sasa sisi Tanzania tulikaa na kuamua je, tunangoja mtu umevaa suti yako usukumwe kwenye bwawa la kuogelea au unajiandaa ukiwa na nguo za kuogelea?

“Tukasema sisi Tanzania tusisubiri kusukumwa kwenye dimbwi la maji, tukaamua tuunde tume tuliyounda wakati huo, ilikuwa ni Tume ya Nyalali,” anaeleza, tume hiyo waliituma iende kuwaletea ripoti ya hitaji la Watanzania.

“Kwa kweli ilikuwa fupi na hatukujaribu kuweka madoido mengine, tukasema akatuletee mawazo ya wananchi wanataka vyama vingi au kimoja, Mwaka 1992. Nyalali alirudi na kuleta ripoti yake.

“Sasa mimi wakati huo nikiwa Waziri Mkuu na ripoti hiyo ikaangaliwa sana na serikali. Tulimshukuru sana Nyalali kwa kuleta ripoti isipokuwa Nyalali akaongezea vitu vyake mwenyewe.

“Kwa mfano akasema kuna sheria 40 zinahitaji kubadilishwa, tukasema hizo sheria 40 alizosema zilikuwa ni sheria ambazo Jaji Mkuu akae atengeneze marekebisho zitapita.

“Kwa hiyo, ripoti ile ilikuwa na mapendekezo ‘chungu mzima,’ kwa mfano kulikuwa na mapendekezo ya serikali ya mpito. Tukafikiri Nyalali alitaka tutengeneze serikali ya mpito... ‘yeye ndio awe Rais’.

“Tukasema hii ni kujaribu kuiyumbisha serikali ya CCM kitaalamu, tukasema tunataka turudi kwenye jambo tulilomtuma,” anaeleza.

Malecela anasimulia kwamba, majibu ya ripoti kwenye suala walilomtuma, Nyalali ilionyesha



Waziri Mkuu Mstaafu, John Malecela. **PICHA: MTANDAO**

INAENDELEA UK.10





# Wanafunzi Kibaha wakaa kwenye nyasi kupata mlo

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

SHULE ya Sekondari ya Wavulana ya vipaji maalumu Kibaha mkoani Pwani inakabiliwa na uhaba wa viti na meza na kusababisha baadhi ya wanafunzi kukaa kwenye nyasi nje ya bwalo wakipata mlo.

Hayo yalibainishwa juzi na Mkuu wa shule hiyo, George Kazi, wakati akitoa taarifa kwenye mahafali ya 56 ya kidato cha nne tangu kuanzishwa kwa shule yao.

Kazi, alisema upungufu wa meza na viti kwenye shule hiyo yenye wanafunzi 809, umekuwa ukisababisha kero kwa wanafunzi hao kukaa chini wanapokula chakula.

Alitaja tatizo jingine linaloikabili shule hiyo ni ukosefu wa kompyuta 100 kwa ajili ya wanafunzi kupata mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

Alwaiomba wadau wa elimu na wazazi kuendelea kushirikiana na serikali kuchangia michango ili kupunguza changamoto zinazoikabili shule hiyo ili kuzidi kuinua kiwango cha elimu kwa wanafunzi na wahitimu wake.

Katika risala yao, wahitimu 104 wa kidato cha nne, walisema shule hiyo, inakabiliwa na uhaba wa vifaa vya maabara na kuwa kikwazo kwa mafunzo kwa vitendo hususani masomo ya sayansi.

Kaimu Mkurugenzi wa Shirika la Elimu Kibaha, Anathe Nko akizungumza kwenye mahafali hayo, aliwaomba wazazi, walezi na wadau wa elimu kuendelea kutoa michango kutatua changamoto zinazoikabili shule hiyo.

Diwani wa Tumbi, Raymond Chokala, alisema changamoto zinazoikabili shule hiyo ameanza kuzishughulikia kwa kutoa viti.

Mwenyekiti wa Bodi ya shule hiyo, Julius Magai, aliishukuru Serikali kwa kuendelea kutoa fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu katika shule na kupunguza uhaba uliokuwepo awali.

Shule hiyo tangu kuanzishwa 1965, imetoa viongozi mbalimbali serikalini, akiwemo Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Mrisho Kikwete, Spika Mstaafu wa Bunge, Job Ndugai, Naibu Waziri wa Afya, Godwin Molel na Naibu Waziri wa Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia, Omari Kipanga.



Mwenyekiti wa Chama cha Msingi cha Itegamatwi Wilaya ya Urambo mkoani Tabora, kinacho jishughulisha na kilimo cha tumbaku, Umaiya Musoma, akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, kuiomba serikali iingilia kati changamoto inayowakabili ya kukosa bembejeo kwa ajili ya kilimo hicho baada ya kudaiwa kutelekezwa na benki inayowadhamini. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mtoto aliyeuawa azikwa, shekhe akemea

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MWILI wa mtoto Mariam Juma (12), Mkazi wa Mrombo jijini hapo, anayedaiwa kuuawa kwa kukatwakatwa na kitu chenye ncha kali kisha kuwekwa kwenye kalai uvunguni mwa kitanda, umezikwa eneo la Mlima CCM ulioko Kata ya Muriet.

Katika maziko yake yaliyofanyika jana, Shekhe wa Msikiti wa Ramadhan wa kwa Morombo, Mohamad Nuru, alikemea baadhi ya watu kuhusisha na mauaji hayo na dini yao.

"Uhalifu hauna uhusiano na dini yoyote nimesikia kwa masikio yangu baadhi ya waombolezaji wakisema wanawake wanaovaa ushungi, wana roho mbaya wanajifunika kumbe ndio wauaji. Ndugu zangu uhalifu hauna uhusiano na dini yoyote," alisema.

Alisema dini yao haiwatumi watu kufanya unyama kama huo bali ni tabia ya baadhi yao na kwamba hakuna uhusiano wa dini na mauaji hayo.

"Kwa sasa kuna mauaji yanatokea maeneo mbalimbali mkoani humu lakini sio wote wa dini yetu bali wa dini nyingine pia wapo na viongozi wao wapo wa dini lakini hakuna kiongozi anayemtuma mtu kufanya uhalifu," alisema.

Alisema kabla ya kutupa lawama kwa dini au kundi fulani ni vema wakajitafakari kwanza ili kuepuka kuleta mtafaruku katika jamii.

"Sisi tunakemea kitendo kilichofanywa na mwanamke huyu, zamani watu walioonekana wenye roho ngumu na chafu ni wanaume, lakini sasa sababu ya haki sawa imesababisha roho za wanaume kuhamia kwa wanawake," alisema Shekhe huyo.

Diwani wa Kata ya Sokoni 1, Saluni Olodi, aliwaomba wananchi kuepuka kurusha lawama kwa baadhi ya dini kuhusiana na mauaji hayo kwa kuwa uhalifu hauna dini.

"Natoa pole kwa familia kwa msiba huu na tusihusishe na dini yoyote hata ukienda gerezani utakuta wahalifu wengi wa dini mbalimbali," alisema diwani huyo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Justine Masejo, alithibitisha kutokea tukio hilo lililotokea Oktoba 12, mwaka huu majira ya mchana katika eneo la Mrombo.

"Mtoto huyu alikuwa ametumwa dukani toka asubuhi lakini hakurejea na ilipofika mchana wazazi wake walianza kumtafuata maeneo mbalimbali baada ya kuingiwa na wasiwasi," alisema.

Masejo, alisema hadi sasa wanawashikilia watu watatu, akiwamo mwenye nyumba ambako mtoto huyo inadaiwa alikutwa ameuawa kwa kuchinjwa.

Mtoto huyo, ameuawa akiwa ni mwanafunzi wa darasa la tano shule ya Dominion iliyoko Morombo.

## MALECELA, 1934 -2024 NINA YAFUATAYO

**INATOKA UK.9**

asilimia 20 walitaka chama kimoja kiondolewe na viruhusiwe vyama vingi na asilimia 80 walitaka chama kimoja tu, kwamba CCM iendelee.

"Sasa hii ikaletwa kwenye serikali na Waziri Mkuu, tukapeleka kwanza kwenye chama (CCM) tukazungumza na kukubaliana kuwa ingawa Nyalali ameleta mapendekezo kwamba Watanzania asilimia 80 hawataki vyama vingi, lakini tuingie kwenye vyama vingi na hawa asilimia 20 waliotaka vyama vingi tuwakubalie.

"Kwa kweli tulifikiria pengine ndio itakuwa njia nzuri na mimi kwa sasa nikikaa na kuangalia nyuma, naona kwamba ulikuwa ni uamuzi wa busara sana, tukaingia kwenye vyama vingi," anasema.

Anasema baada ya kuingia kwenye vyama vingi, anawaeleza watu walikuwa na makeke kwamba wataiondoa CCM madarakani mapema, nako akiwa na simulizi yake:

"Watu walikuja na makeke kuwa wataiondoa CCM madarakani kesho tu. Tukumbuke wakati huo mimi nilikuwa Waziri Mkuu, Makamu wa kwanza wa Rais na Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa. Tukapambana hawa waliokuwa wanasema wanataka kutung'oa kwa kweli mwaka 1992 tulipambana," anasema.

### UPIGAJI KURA

"Utaona tangu mwaka ule, mara nyingi watu watakwambia 'CCM wanaiba kura', mtindo wetu wa kupiga kura...Mimi niliangalia nchi zote za Afrika wenye mfumo mzuri wa kupiga kura ni Ghana, nikatoa mapendekezo Tanzania tukubali utaratibu wa Ghana.

"Utaratibu ni kwamba kila kituo kiwe na wapigakura 300, wanapopiga kura sanduku linawekwa eneo la wazi, halafu wawakilishi wa vyama wanakuwa wanazunguka sanduku.

"Kwa hiyo, watu wanakuja wanapiga kura kila mtu anaangalia, ikifika saa 10 mnalifunga sanduku palepale, wale wawakilishi wa vyama vingine wapo,"anasema.

Anafafanua baada ya hapo wanapeleka kwenye chumba wakiwa na wawakilishi wa vyama na kura zinahesabiwa kwa kuangalia kila wakala anapewa za chama chake kuzishika.

Analalamika "ulimwenguni kila anayeshindwa humwambia mwenzake ameiba". Lakini, kwa upande wa CCM walifanya kila kitu kuepuka mashtaka ya kuiba kura.

"Nafikiri pamoja na hayo, sidhani kama utapata mfumo mzuri zaidi ya huo na kama itapatikana ya kuboresha, pia itakuwa vizuri zaidi utaona mfumo huu unaruhusu uwazi na ukweli kwenye mchakato wa upigaji kura,"anasema, akisifu tangu kipindi hicho mfumo wa vyama vingi umekuwa na tija.

Nipashe
# TESA
Jumanne Oktoba 15, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI







Viongozi na wananchi jipekueni ni wazalendo




Uhuru na demokrasia, hekima iliyoiacha ilivyo na nafasi enzi hizi za vyama vingi

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

KUMBUKIZI YA NYERERE

# Ndivyo wengi wanavyomwangusha wamekimbia maarifa, kujielimisha

• Wanaamini zaidi ushirikina mafanikio bila kazi na kufoji

BABA wa Taifa Julius Nyerere alikuwa mwalimu kweli akiwafundisha wanafunzi ambao ni Watanganyika na baadaye Watanzania.

Taifa hili lilikuwa 'darasa', analolifundisha, kila kitu kuanzia kusoma, kuandika, kuhesabu, kulima, kutunza afya zao na kuwa na umoja.

Akiwa mwalimu, Nyerere hakutaka taifa lenye watu wajinga akaanzisha na kutekeleza mipango mbalimbali ya elimu kuanzia, ya msingi hadi ya watu wazima miaka hiyo ikiitwa ngumbaru.

Akiamini kuwa elimu ni haki ya kila mtu, alifanya juhudi zote kuwaelimisha watoto hadi watu wazima mijini na vijijini na hata 'madongo kuinama' msamiati unaomaanisha ni sehemu ambazo hazifikiki.

Pamoja na juhudi hizo, Nyerere alitamani kuona Tanzania ambayo elimu inatoa nafasi kwa yeyote mwenye uwezo kusoma hadi kufanikiwa.

Kwa njia hiyo aliandaa mipango ya watu kusoma bila kujali kama ni maskini au matajiri. Kwa msingi huo, wengi ambao wasingeweza kulipia masomo walisoma hadi vyuo vikuu na kufurahia matunda ya elimu bure.

Mwalimu alikuwa mzee wa fikra 'tunduizi' alitamani Watanzania wanaposoma wajengeke kielimu



wawe wadadisi wa mambo na kutafuta kujua na kusoma zaidi.

Katika maono yake alitaka elimu iwe nyenzo ya kumkomboa Mtanzania tofauti na elimu ya kikoloni, ambayo ilikuwa inaendeleza fikra za utegemezi, kudhalilishwa.

Ni elimu iliyomfanya raia kuwa mtumwa wa kumtumikia Mzungu au Mwarabu ama Mhindi na ikiwa na kasoro ya kujiona kuwa ukiwa na elimu kiasi juu ya Waafrika wenzako.

Kwa maana nyingine Mwalimu Nyerere alitamani kupata elimu inayoleta kizazi cha watu wenye tabia ya kuheshimiana na siyo wenye kiburi na wanaojiona kuwa ni wasomi tena waliowazidi wote.

Kwa Mwalimu Nyerere elimu ilikuwa si nadharia ambayo ni kusoma vitabu na maandishi ya walimu ubaoni bali pia kuchanganya nadharia na vitendo.

Kuanzia miaka ya 1970, shule nyingi zilikuwa na mashamba ya kilimo na kuzalisha mazao mbalimbali kuanzia mboga, ya chakula na ya biashara.

Kadhalika, kulikuwa na ufugaji wa wanyama mbalimbali, na kazi za kujitegemea kama ufundi na useremala ili kufikia azma ya elimu na kujitegemea.

Alitamani wasomi kuujua ufundi ili vijana wafahamu mengi zaidi ya kusoma vitabu darasani na kujibu maswali, alilenga pia skili hasa kazi za mikono ambazo ni njia moja ya kujenga msingi wa kujitegemea kwa mahitaji ya mwanafunzi.

**KISOMO KWA WAZEE**

Mwalimu Nyerere alifundisha kuwa elimu haina mwisho wala haikwamishwi na umri ndipo, anapowahimiza watu wazima kusoma pia na kujibidiisha kusaka elimu kupitia mpango wa kisomo cha elimu ya watu wazima.

Ni katika miaka ya 1970 Mwalimu mbali ya kushughulikia elimu ya watoto na vijana darasani na vyuoni, alianzisha mpango wa elimu ya watu wazima.

Wazee walisoma bila kujali wapo mijini au vijijini na walipata fursa ya kujiongezea ufahamu kuanzia kujifunza kukaa darasani, kusikiliza walimu, kusoma na kuandika, kuhesabu kujua lugha hadi kufikia maarifa mengine ya juu katika fani na taaluma mbali mbali.

Mwalimu alianza kuiongoza nchi ambayo wananchi wengi walikuwa hawajui kusoma chochote hata noti au sarafu ya fedha.

Kuanzia wakulima, wafugaji, wavuvi, wapasua mbao, walinzi kwenye ofisi za serikali, maseremala na viongozi wa serikali mitaani na vijijini walikuwa hawajui kitu.

Kupitia kisomo cha watu wazima aliwahimiza kujiandikisha vituoni na kusoma kwa bidii. Aidha, walihimizwa kujiongezea ujuzi kwenye fani na shughuli zao ili kuboresha maisha na kubadilisha maisha yao.

Vitabu vilichapishwa katika fani za aina nyingi ambavyo viliwapa watu fursa ya kujifunza kusoma na pia kujiongezea maarifa na ujuzi wa kila aina.

Walijifunza kuanzia mapishi, ufugaji wa kisasa, kilimo cha mashamba na bustani, kujenga nyumba bora na ushonaji.

Kama ni mvuvi alijiongezea

INAENDELEA UK. 14

ELIMU

NA RAHMA SULEIMAN, ZANZIBAR

# Viongozi na wananchi jipekueni ni wazalendo mnaishi kanuni zake, vipi tamaa ya mali, ubadhirifu

NI miaka 25 tokea Tanzania lilipompoteza mwasisi wake Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, Oktoba 14, 1999 akiwa kwenye matibabu kwenye Hospitali ya Mtakatifu Thomas huko Uingereza.

Alipotwaliwa wapo baadhi ya watu walisema huenda Tanzania inekumbwa na hali ya kutokuelewana na kuvutana katika baadhi ya mambo na hata wananchi kugawanyika.

Hilo halijawezekana kwani baada ya miongo miwili na nusu sasa hakujawa japo hata na ishara ya kutokea mpasuko wa kitaifa au mgawanyiko, badala yake Tanzania imezidi kuwa moja na kupata mafanikio makubwa kisiasa, kiuchumi na kijamii.

Pamoja na kwamba miaka 23 ya utawala wa Mwalimu Nyerere taifa lilikuwa likifuata mfumo wa chama kimoja, hata pale viliporuhusiwa vyama vingi, nchi imebaki katika mshikamano.

Kwanini basi hakujawa na mgawanyiko, mpasuko au utengano wowote? Hakuwezi kutokea na yote hayo kwa kuwa waasisi wa taifa hili, Mwalimu Nyerere na mwenzake Sheikh Abeid Amani Karume, waliweka misingi, miiko, uadilifu na kanuni za kudumisha mtangamano.


Ndiyo maana hata alipoingia madarakani Rais wa Awamu ya Pili, Mzee Ali Hassan Mwinyi, taifa limeendelea kubaki vilevile bila kutikisika au kushtushwa na lolote.

Licha ya waasisi hao kuondoka duniani wakiacha nchi ikiwa moja, yenye katiba zake, kanuni, taratibu, miiko na miongozo kama nguzo na kinga zinazolinda usalama wa taifa, watu na utamaduni mmoja.

Nyerere ambaye amekufa miaka 25 iliyopita ameiacha Tanzania ikishikamana bila ukabila, udini, ukanda wala ubaguzi wa ina yoyote.

Amewaacha Watanzaia wakiitana ndugu. Kila mmoja akiheshimu ubinadanu na utu wa mwenzake, kuthamini heshima ya kila mmoja, kusaidiana na kuhurumiana. Watanzania hawajivunii dini, kabila wala rangi zao.

Katika muda wote wa miaka ya uongozi wake, Mwalimu Nyerere alisimamia misingi ya uongozi na kuwataka viongozi katika nafasi zao kutambua kuwa binadamu wote ni sawa.



Alikuwa akisema mara kwa mara katika maisha ya uongozi wake wakati wa kupigania uhuru na hata baada ya kujitawala kuwa, kila mmoja anastahili kuheshimu wenzake na kuheshimiwa pia, akithamaniwa na kutambuliwa utu wake.

Nyerere hakuwa mtetezi wa haki za binadamu kwa Tanzania peke yake bali akipaza sauti yake kimataifa. Kila mahali duniani ambako binadamu walibaguliwa na kutengwa, Mwalimu hakusita kuwasemea.

Wakati Tanzania kila mwaka wamekuwa wakimkumbuka mwasisi wao, duniani kwenye midahalo na mijadala mbalimbali, kiongozi huyo hukumbukwa kwa uongozi wake bora uliosifika hasa usiothamani mali na utajiri.

Nyerere na mshirika mwenzake Karume ndio waliokuja na wazo la kuyaunganisha mataifa ya Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964 na kuundwa kwa taifa ambalo halikuachwa na wakoloni liitwalo Tanzania.

Mwalimu Nyerere hakuishia hapo lakini pia alihakikisha mataifa yote ya kusini mwa Afrika yaliokuwa yakitawaliwa kibabe na wakoloni nayo yanajikomboa na kujitawala.

Akaweka mkazo mkubwa wa kuhifadhi vyama vya ukombozi kwenye ardhi ya Tanzania, wapigania uhuru wake hadi pale walipopata uhuru katika nchi zao.

Kiongozi huyo ndiye aliyeweka mkazo na kuhakikisha inaundwa Jumuiya ya Afrika Mashariki mwaka 1967 kati ya Tanzania, Kenya na Uganda ingawa baadhi ya viongozi wenzake hawakutaka mpango huo.

Zikazuka fitna, mizengwe na kila aina ya hila zilizotaka jumuiya hiyo ife. Kweli ikafa miaka 1977 na mataifa wanachama wakarudi nyuma kimaendeleo baada ya mafanikio makubwa waliyoyapata kupitia mtangamano.

Hata hivyo baada ya kupuuza mawazo ya Nyerere, viongozi walikuja kuongoza madola baadaye mwaka 1999 wakaanzisha tena mchakato wa kuunda Jumuiya ya Afrika Mashariki kama alivyotaka Nyerere miaka mingi iliyopita safari hii ikiwa na mataifa mengi zaidi.

Mbali na Kenya, Uganda na Tanzania imezileta pamoja Rwanda, Burundi, Congo, Sudan Kusini na Somalia.

Nyerere ametwaliwa, hatunaye tena, hatarudi lakini fikra zake, maono na mawazo yake, yataendelezwa kwa bidii na kila rais au utawala utakaoshika madaraka kwakuwa taifa hili lina misingi, asili na miiko ambayo ilianzishwa na waasisi hasa yeye na Karume.

Mwalimu alichukia unyonyaji, uonevu, kukandamiza haki za wanyonge, unyanyasaji lakini pia hakuwa kiongozi aliyependa upendeleo.Akichukia rushwa, ubadhirifu wa mali za umma na matumizi mabaya ya rasilimali za taifa.

Kiongozi huyo atakumbukwa kwa uongozi wake ambao hakuonyesha hata mara moja anahamanika na kutaka utajiri, hakuwa mkwapuzi wa mali za umma wala kujilimbikizia mali kama ilivyokuwa kwa baadhi ya viongozi.

Mwalimu Nyerere akiamini katika nadharia ya uongozi si ajira inayohitaji malipo lakini pia aliamini kila binadamu yuko huru kuchagua anachokiamini alimradi jambo hilo halivunji sheria za nchi wala katiba.

Taifa linapokikumbuka kifo chake, lazima viongozi wajipekue, Watanzania pia wajichunguze endapo bado wanaishi katika ndoto zake hizo au wameziacha kanuni hizo na sasa wanakwenda segemnege, shaghalabaghala au ndivyo sivyo.

KUMBUKIZI YA NYERERE

ELIMU

NA DK PETER KAFUMU

# Uhuru na demokrasia, hekima iliyoiacha ilivyo na nafasi enzi hizi za vyama vingi



Mwalimu Julius Nyerere (katikati) na Joan Wicken (kulia), aliyekuwa msaidizi wa Mwalimu na Malkia Elizabeth wa Uingereza. Wote ni marehemu. **PICHA: MTANDAO**

TUNAPOKUMBUKA miaka 25 tangu Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, atuache ni muhimu kutafakari hekima aliyotuachia, inayotuongoza kuelekea mafanikio.

Wiki hii taifa bado linalia likimkumbuka kiongozi wake mkuu aliyehakikishia kila raia wake anapata haki, uhuru na ulinzi wa maisha yake bila kujali dini, rangi, kabila na hata itikadi za kisiasa. Mwalimu Nyerere alikuwa ngome ya ulinzi kwa watu wengi hasa maskini na wasiojiweza.

Leo tunaendelea kumuenzi Baba wa Taifa kwa sababu ya hekima na upendo alioturithisha watu wake, vitakavyodumu hadi mwisho wa nyakati. Ni muhimu wakati wote tumuenzi kwa kutafakari maono, matumaini na matamanio yake kwanza kiongozi, uhuru na demokrasia.

Hekima ya Mwalimu Nyerere kwenye maeneo hayo matatu iliongozwa na imani yake kwenye aina ya demokrasia ndani ya chama kimoja inayompa kila raia nafasi ya kuwa huru kushiriki katika kujiletea maendeleo na kulindwa.

Alitamani sana Tanzania iwe na demokrasia inayowahakikishia uwepo wa haki na uhuru wa watu.

Makala inamtafakari kuhusu sehemu ya hekima aliyotuachia katika kitabu chake cha "Binadamu na Maendeleo" alichokiandika mwaka 1967, akitoa mafundisho mahususi kuhusu umuhimu wa uongozi, uhuru na demokrasia kwa maendeleo ya watu.

Anaeleza kuhusu umuhimu wa demokrasia ya chama kimoja inayohakikisha uhuru wa kushiriki katika maamuzi ya kidemokrasia ili kuleta maendeleo endelevu ya watu.

Anasema "...kuna mambo mawili muhimu katika maendeleo ya watu. Jambo la kwanza ni uongozi thabiti unaotoa elimu, la pili ni demokrasia katika maamuzi. Kwa sababu uongozi haumaanishi kuwapigia kelele na kuwashurutisha watu; kuonea watu au kikundi cha watu unaotofautiana nao; na zaidi sana haimaanishi kutoa amri kwao ili wafanye lile au hili.

"Uongozi unamaanisha kuongea na kujadiliana na watu ili kuwaeleza na kuwaelewesha. Aidha, unamaanisha kutoa mapendekezo yanayojenga na kuwahamasisha watu kufanya kazi kwa vitendo kuhusu kile ulichowaelekeza au kuwaomba wafanye kama kiongozi wao. Uongozi unamaanisha kuwa mmoja wa wale unaowaongoza na kujitambua kuwa wewe uko sawa nao kama mtumishi wao..."

Mwalimu katika kitabu hiki anasisitiza kuwa mamlaka ya uongozi uliyopewa hayana maana kuwanyang'anya watu mamlaka yao. "...Watu lazima wafanye maamuzi yao wenyewe kuhusu maisha yao kwa kufuata njia za kidemokrasia. Uongozi hauwezi kuchukua nafasi ya demokrasia; lazima uwe sehemu ya demokrasia. Kama uamuzi utahusu mambo ya taifa zima basi watafanya uamuzi huo kupitia halmashauri kuu na bunge...

Kama jambo lenyewe linahusu maisha yao kwa mfano kujitolea kuhusu mradi wa maendeleo, watu wanaohusika lazima wafanye maamuzi yao kwa majadidiliano na uhuru. Hakuna namna nyingine maendeleo yanaweza kupatikana..."

Mwalimu aliamini katika kanuni za msingi za kidemokrasia zinazolinda na kuendeleza uhuru na umoja wa taifa. Kwenye demokrasia anasema msingi wa kwanza ni uhuru wa kujieleza na wa pili ni dhamu ya kutekeleza maamuzi yaliyofikiwa kidemokrasia. Aliandika hivi: "...Kuna mambo mawili muhimu katika demokrasia, ukiyakosa hayo demokrasia haipo. La kwanza ni kila mtu ni lazima kusema kwa uhuru na maoni ya kila mmoja lazima yasikilizwe. Hata kama mawazo ya mtu huyo hayapendwi kiasi gani, au walio wengi wanamdhania amepotoka, si kitu.... Kila Mtanzanzania, awe wa kijijini, mjumbe wa halmashauri ya wilaya, mbunge aweze kusema kwa uhuru bila hofu ya vitisho - ama katika mkutano ama nje ya mkutano..."

Mwalimu pia alieleza kuhusu haki ya wachache katika demokrasia, akiandika: "...Watu wenye mawazo tofauti hata wakiwa wachache, lazima wawe na haki ya kutoa mawazo yao katika majadiliano bila ya hofu ya kusumbuliwa, mawazo yao na yashindwe katika hoja ya majadiliano, siyo kwa vitisho na mabavu...."

Hajasahau haki ya walio wengi kwenye demokrasia kwa kusema: "... Kadhalika wale walio wengi lazima wawe tayari kuyashikilia mawazo yao mpaka wale wachache waaridhike kuwa uamuzi uliofanywa kwenye jambo lile ulikuwa sawa. Majadiliano lazima yaruhusiwe kuendelea kwa uhuru.. .

Hekima ya Mwalimu inaendelea kuelekeza kuwa kama katika majadliano yenye usawa na kila maoni yametolewa uamuzi lazima ufikiwe na walio wengi lazima wafuatwe. Mwalimu anamalizia kwa msemo huu: "...Maana kama vile walio wachache walivyo na haki ya kusikilizwa, wengi wanayo haki ya kufuatwa...".

Msingi wa pili wa demokrasia kwa maelezo ya Mwalimu ni uwezo wa kushikilia uamuzi uliopatikana katika majadiliano ya kidemokrasia. Akisema"...Uamuzi ukishafanywa lazima ukubalike kuwa ni wa watu wote, na wote hata wale waliokuwa wakipinga hawana budi kushiriki katika kutimiza jambo hilo...

"Aidha, walio wachache lazima waruhusiwe kutetea mabadiliko katika sheria au katika maamuzi. Lakini kwa sasa lazima watii sheria iliyopo mpaka hapo watakaofaulu kuwashawishi walio wengi kukubali mabadiliko hayo. Bila utaratibu wa namna hiyo maendeleo ya aina yoyote hayawezekani..."

Hekima ya Mwalimu Nyerere kuhusu uongozi na demokrasia inapita ufahamu wa kawaida na ni hazina inayoweza kutumulikia njia ya kusonga mbele kama taifa. Katika demokrasia ya vyama vingi tunayoitekeleza leo, hekima hii ya kutoa uhuru bila ubaguzi kwa watu kushiriki maamuzi na pia kwa viongozi kuongoza watu wakiwa watumishi wa watu, inafaa kuigwa.

Kanuni mbili muhimu alizotuachia Baba wa Taifa za uongozi, uhuru na demokrasia ambazo ni kiongozi kuwa mtumishi wa watu na siyo mnyampara, na kanuni ya pili ni kuwepo kwa uhuru binafsi wa kutoa maoni na mawazo mkutanoni au nje ya mkutano katika kujiletea maendeleo bila kubaguliwa au kutishwa kutokana na rangi, dini, kabila, chama cha kisiasa au kikundi kingine nayo ni ya muhimu kuzingatiwa.


Tunapotafakari hekima na mafundisho yake ni muhimu kuiruhusu alichotufundisha kutanda juu yetu na kutufunulia ufahamu, elimu na uelewa wa kuongoza taifa letu kwenda kwenye neema na heri. Ufahamu na elimu hii tunahitaji kuichambua na kuitohoa ili iendane na wakati tulio nao.

Mwalimu Nyerere alilinda taifa letu na limestawi hadi leo. Tuendelee kumuenzi Baba yetu kwa kutafakari maoni na mafundisho yake na kuyaishi kadiri ya wakati tuliomo.

***Mwandishi ni mbunge wa zamani wa Igunga na Kamishna wa Madini mstaafu.***



Familia ya Mwalimu Nyerere ikiongozwa na mjane Mama Maria pamoja na watoto wake wakiaga mwili wake, kabla ya mazishi yaliyofanyika kijijini kwake Butiama. **PICHA MTANDAO**



# MWALIMU TWAKULILIA

1. Mwalimu huko mbinguni, chungulia natazama,
   Wanao duniani, uliyetuacha nyuma,
   Tumekuwa maskini, tukitamani kiama,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

2. Baba tumechoka, kulia kuomboleza,
   Rushwa imejisimika, mwili kutukandamiza,
   Sisi tumetatizika, twaona mbeleni kiza,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

3. Twalia tukitamani, uje na fimbo ya chuma,
   Na tena wanatamani, uje na nguvu kinoma,
   Na upanga mkononi, ukasitishe dhuluma,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

4. Rushwa kweli imeshamiri, Bara hataVisiwani,
   Imezidi kuathiri, wazee kwamaskini,
   Athari zimekithiri, tumechoka mtimani,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

5. Hakuna uandilifu, rushwa imetapakaa,
   Viongozi wanasifu, rushwa waishangilia,
   Wametubana mapafu, vigumu kupumulia,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

6. Ufisadi wa hatari, meibuka kwa ukali,
   Udhalimu ulokithiri, ndiyo ufisadi mkali,
   Unatutesa chakari, mechoka na hii hali,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

7. Rupia imetawala, ni tamu kama asali,
   Mafisadi ni wakala, kufanya siasa kali,
   Wana sumu kama swila, wenye nazo ni wakali,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

8. Maisha mekuwa chini, yamezidi kuzizima,
   Hongo mekuwa hadharani, kila mtu anachuma,
   Uozo jamiini, mimbarini kusimama,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

9. Mekufa matumaini, yamaisha ya heshima,
   Wanao tunatamani, urudi wako mtima,
   Ili haki na amani, vibaki nasi daima,
   Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

10. Tamati nimefikia, Mwana Shilinde napisha,
    Ni leo twakumbukia, mwisho wa yake maisha,
    Daima takumbukia, yale ulotufundisha,
    Mwalimu twakulilia, twatamani ungerudi.

**Dk. Peter D. Kafumu**
**(Ngw'izukulu Shilinde)**

## NDIVYO WENGI WANAVYOMWANGUSHA WAMEKIMBIA MAARIFA, KUJIELIMISHA

**INATOKA UK.11**

maarifa zaidi kuhusu kazi yako. Kadhalika mkulima alijizatiti kufahamu kuhusu kilimo cha kisasa, matumizi ya mbolea, viuatilifu na kuacha kulima kizamani.

**TULIKWAMAJE?**

Ndiyo maana leo Watanzania wanapogeuka nyuma na kuangalia kazi na kampeni za Mwalimu tafakari inakuwa.

"Kama Watanzania tungetii na kufuata maelekezo ya Mwalimu, mambo leo yasingekuwa kama yalivyo. Tungekuwa mbali kimaendeleo, na tungekuwa na mategemeo ya kufanikiwa zaidi kama ambavyo China na nchi nyingine za Asia zimefanikiwa.

Miaka 63 ya Uhuru na 25 ya kifo cha Nyerere wapo watu wasiotaka kuelimika kama Mwalimu alivyotamani. Hawawapeleki watoto shule. Kuna baadhi wanashiriki kuwalazimisha wasichana wadogo kuingia kwenye ndoa badala ya kuwa darasani.

Leo ni zama za utandawazi, elimu hasa masuala ya kielektroniki na kidijitali ndiyo inayoongoza dunia lakini Watanzania wengi hawana elimu wala ujuzi wa masuala muhimu ya msingi mfano jinsi ya kutumia dawa kujitibu. Watanzania wengi hawataki kujielimisha hata kusoma gazeti hawana muda. Ari ya kujielimisha inapungua sana na wengi wanashindwa hata kuandika majina yao licha ya kumaliza sekondari.

**KUFOJI VYETI**

Wanadaiwa wako wasomi, lakini walisaka vyeti badala ya kusoma darasani. Wanashikilia vyeti vya shahada za uzamili na uzamivu lakini hawakusoma kuna waliowafanyia mitihani na kuwaandikia tasnifu. (Dissertation).Taifa linadaiwa kuwa na wasomi lakini 'vihio' au mbumbumbu licha ya vyeti vyao kuwa na AAAA wakiita misonge au banda pamoja na B+ ambao kiwango cha ufaulu ni zaidi ya 91/100.

Zipo familia zinanunua vyeti au kutumia vyeti vya ndugu zao kwa kubadilisha majina au kufanya chochote kinachowezekana kuwasaidia watoto wao kupata maisha hasa ajira.

**USHIRIKIANA**

Watanzania wamezidi kumwangusha Baba wa Taifa, aliyetamani wawe na maarifa mfano ni aibu kuamini kuwa utajiri au madaraka yanapatikana kwa kuua albino, kunajisi watoto na kutumia tunguri.

Hata watoto wadogo wanaaminishwa kuwa njia ya mafanikio ni kupitia ushirikina na wapo mahiri wa kuvaa hirizi na kubeba dawa wanazopewa na wazazi au walezi ili wafaulu mitihani na kufanikiwa kimaisha.

Vijana wanaishi vijiweni na kusaka utajiri kwa waganga ambao wanabandika mabango kuwa wanaweza kuongeza utajiri, kutakatisha nyota na kupatia mteja fedha za majini.

Leo ni kama taifa limejaa watu waliojisahau badala ya kujiongezea maarifa katika fani na shughuli unazofanya kama kilimo, ualimu uandishi wa habari, daktari, uashi, umakenika, uvuvi au mamalishe wanategemea ndumba.

Hakuna mwenye hamasa ya kununua vitabu, kugharamia mafunzo kama semina badala yake tunataka kulipwa tunapopewa elimu au mafunzo.

Kurejea nyuma kwenye imani kuwa mafanikio yanatokana na ushirikina ni aibu na kumwangusha Mwalimu Nyerere ambaye alitamani kila mmoja awe na maarifa na ayatumie kubadilisha maisha yake na kuleta maendeleo ya taifa.

Watanzania wanapoukumbuka mchango wa Mwalimu kwenye maendeleo ya taifa, hebu watafakari njia zao, hasa kwenye elimu kwa kutafuta maarifa badala ya ushirikina, kufoji vyeti na kuacha kujielimisha kwa manufaa binafsi na taifa.

## Halmashauri kuendesha miradi ya kimkakati

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imezindua mwongozo wa uanzishaji na usimamizi wa kampuni za uendeshaji wa vitega uchumi kwa halmashauri ili kuwa na miradi ya kimkakati yenye tija.

Akizindua mwongozo huo mwishoni mwa wiki iliyopita jijini hapa, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Adolf Ndunguru, alisema umeandaliwa kwa ushirikiano baina yao, Wizara ya Fedha na Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF).

Ndunguru, alisema hatua hiyo ni zana mpya ya marejeo kwa timu za miradi za halmashauri ambao unatoa mwongozo wa hatua kwa hatua ya jinsi ya kusimamia miradi ya kimkakati ya kuzalisha mapato kwa kutumia kampuni.

"Mwongozo huu ni suluhisho la changamoto ya sasa ya halmashauri katika miradi ya kusimamia vitega uchumi kwenye eneo la utawala, uendeshaji na usimamizi wa fedha," alisema.

Alifafanua kuwa kwa mwaka 2017/18, serikali imewekeza zaidi ya Sh. bilioni 294.96 kwenye miradi 46 ya kimkakati, kati ya hiyo 26 imekamilika.

Hata hivyo, alisema imebainika kuwa mamlaka hizo zinakabiliwa na usimamizi duni wa miradi, ukosefu wa wataalamu na kushindwa kukamilka kwa wakati huku mingi ikitekelezwa chini kwa kiwango.

"Naomba watendaji wote mkasimamie vizuri mwongozo huu ikiwamo kutoa mawazo mapya kwa njia za kibunifu za kuimarisha makusanyo ya fedha katika mamlaka ya serikali za mitaa," alisema Ndunguru.

Mkuu wa UNCDF, Peter Malika, alisema shirika hilo limeweka kipaumbele kushirikiana na serikali kusaidia kujenga uwezo wa kuwekeza katika maendeleo ya ndani ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Malika, alisema mwongozo huo umeweka viwango na kuziwezesha halmashauri na taasisi za serikali zinazoendesha biashara kutumia muundo sahihi wa utawala bora ili kuboresha miradi, kutoa huduma bora, kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi na kukuza maendeleo ya ndani ya nchi.

Awali, Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa TAMISEMI, John Cheyo, alisema kuwapo kwa muundo mzuri wa kampuni hizo kutawezesha utekelezaji wa miradi na kufikia malengo yaliyokusudiwa.

Alisema matumaini ya serikali ni kuwa mwongozo huo utaimarisha uwezo wa kitaalamu wa mamlaka hizo katika usimamizi wa miradi ya uwekezaji ya kuongeza mapato na kuleta uwajibikaji.

# Tanzania kusambaza mbolea Afrika

**Na Renatha Msungu,**

DODOMA

TANZANIA imejipanga kuwa kitovu cha usambazaji mbolea katika nchi nane barani Afrika, imefahamika.

Ni baada ya serikali kuzindua mkakati wa maendeleo ya tasnia ya mbolea wa mwaka huu hadi 2030 ili kuhakikisha kila eneo nchini linatumia mbolea kulingana na afya ya udongo wake.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Mweri, akizungumza kwenye uzinduzi wa mkakati huo jijini hapa, alisema kuwa pamoja na kuwapo kwa viwanda vya mbolea, kuna mpango wa kuanzisha vingine nchini ili ijitosheleza na kusambaza kwa nchi hizo zinazozunguka Tanzania.

**Msibweteke badala yake mwende kuongeza kasi ili wakulima waongeze jitihada ya kutumia mbolea ya ruzuku kwenye kilimo.**

Mweri, alisema Tanzania inataka kila eneo mkulima atumie mbolea kulingana na afya ya udongo ili kuwa na kilimo chenye tija.

Alisema mkakati huo unaakisi dira ya maendeleo ya taifa ili kutimiza ndoto ya serikali ya kufuta umaskini na kuwa na usalama wa chakula nchini.

Alisema baadhi ya mikoa imeanza kupima afya ya udongo ili kila mmoja awe anatumia mbolea kulingana na hali ya afya ya udongo.

"Kuna maeneo yalikuwa hayavutii kibiashara kutokana na kutotumia mbolea ndio maana serikali imeamua kuwekeza katika mbolea ili kuongeza kasi ya matumizi sahihi ya mbolea," alisema.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA), Joel Laurent, aliishukuru serikali kwa kuwekeza kwenye mbolea ili kuchochea matumizi yake kwa wakulima.

Laurent, alisema kutokana na 'Kampeni ya Kilimo ni Mbolea' inayofanywa na TFRA, wakulima wameongeza mwamko wa kutumia mbolea kwenye kilimo chao.

Mwakilishi wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Jane Jerry, aliipongeza TFRA kwa kushawishi matumizi ya mbolea kwa wakulima nchini.

"Msibweteke badala yake mwende kuongeza kasi ili wakulima waongeze jitihada ya kutumia mbolea ya ruzuku kwenye kilimo," alisema.




Katibu Mkuu Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Adolf Nduguru (wa pili kushoto), akikata utepe kuzindua mwongozo wa uanzishwaji na usimamizi wa kampuni mahsusi za uendeshaji wa miradi ya vitega uchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, jijini Dodoma jana. Kutoka kushoto ni Johnson Nyella, Kamishna wa Sera wa Wizara ya Fedha, aliyemwakilisha Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Mkurugenzi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji nchini (UNCDF), Peter Malika na Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa TAMISEMI, John Cheyo (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NSSF wampa tuzo Samia kwa mafanikio

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MFUKO wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) umempatia tuzo Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufungua milango ya uwekezaji, kuimarisha uchumi na kuchangia kupata mafanikio katika kipindi chake cha uongozi.

Tuzo hiyo ilikabidhiwa na Mkurugenzi Mkuu wa NSSF, Masha Mshomba kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, katika kilele cha Wiki ya Huduma kwa wateja jijini hapa.

Mshomba alitaja mafanikio yaliyotokana na jitihada hizo za Rais Samia kuwa ni pamoja na ongezeko la wanachama hadi kufikia 1,350,000 ikilinganisha na wanachama 750,000 waliokuwapo miaka mitatu iliyopita.

"Pia utoaji huduma kwa wateja umeimarika na sasa mwanachama anaweza kuomba mafao na kulipwa ndani ya saa 24 za kazi kutoka siku 30 au 14 zinazotambulika kisheria," alisema.

Alisema NSSF imeongeza uwezo wa ukusanyaji michango, mapato ya uwekezaji na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na kurahisisha utoaji huduma kwa wanachama.

Kuhusu ucheleweshaji wa michango, aliomba serikali kuendelea kuhamasisha waajiri kutoa kwa wakati ili kuondoa usumbufu ambao umekuwa ukijitokeza kwa maofisa wa mfuko huo na wanachama kufuatilia.

Kwa upande wake, Senyamule aliupongeza mfuko huo kwa huduma bora kwa wanachama wake na kusisitiza kuendelea kutoa elimu kwa wananchi ya umuhimu wa kujiunga na mfuko wao kwa maisha yao ya sasa na baadaye.

"Nimeendelea kuwafuatilia kupitia vyombo vya habari na nafarijika sana ninaposikia mfuko umekua hadi kufikia uwekezaji wa Sh.trilioni nane," alisema.



# Vijana 500 kuajiriwa Makambako

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

KAMPUNI ya Fujian Hexingwang Industry Tanzania.co.Ltd imeanza ujenzi wa kiwanda cha kuzalisha na kutengeneza chuma na magari bunifu ya utalii katika Kijiji cha Ikelu Halmashauri ya Mji wa Makambako mkoani hapa ili kutoa ajira kwa zaidi ya vijana 500.

Uwekezaji wa kiwanda hicho ambacho pia kitakuwa kinatengeneza unga wa chuma, chokaa na saruji, utagharimu zaidi ya Sh. bilioni moja.

**Raia huyo wa Chinga, amewekeza kutokana na Tanzania kuwa nchi ya amani na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji.**

Mpango huo ulitangazwa mwishoni mwa wiki iliyopita na Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni hiyo, Xu Xingda wakati wa mkutano na wananchi na Balozi wa China nchini, Chen Mingjian, baada ya kukagua eneo la ujenzi wa kiwanda hicho.

Xingda, alisema ameanza ujenzi wa kiwanda hicho kutokana na hamasa kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka na serikali kuweka mazingira mazuri na rafiki ya uwekezaji.

"Katika ardhi hii tutajenga kiwanda kikubwa na cha kisasa kwa ukanda wa Afrika Mashariki ili kusukuma maendeleo ya uchumi wa Mkoa wa Njombe na nchi ya Tanzania kwa ujumla," alisema.

Kwa upande wake Mtaka, alisema malengo yake ni kuhakikisha Makambako inakuwa ya viwanda huku akiwaahidi wananchi kiwanda hicho kinajengwa kama alivyofanya kwenye mikoa mingine aliyoiongoza ikiwamo cha chaki Simiyu na mbolea Dodoma.

"Rais Samia Suluhu Hassan alipokuja Njombe nilimwahidi ni lazima tutabadilisha mkoa huu na kwa sababu ameniamini na wenzangu, anapofungua fursa sisi tuna wajibu wa kuzichukua na kuzitafsiri kwenye vitendo," alisema Mtaka.

Balozi Mingjian, alipongeza juhudi za uwekezaji wa kiwanda hicho na kusema utatoa fursa ya ajira za kutosha kwa Watanzania na bidhaa zenye mahitaji makubwa kwa Tanzania na nchi nyingine na kupata fedha za kigeni.

Mbunge wa Makambako, Deo Sanga, alisema raia huyo wa Chinga, amewekeza kutokana na Tanzania kuwa nchi ya amani na kuboreshwa kwa mazingira ya uwekezaji.

Alitoa rai kwa wananchi kusomesha watoto wao ili kutumia fursa ya ajira katika kiwanda hicho.

Mwekezaji huyo alitumia fursa hiyo kukabidhi kompyuta mbili, printa na begi za shule kwa wanafunzi 450 na kuahidi kujenga chumba kimoja cha darasa katika Shule ya Msingi Ikelu.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde, akikabidhi tuzo kwa Mkuu wa Idara ya Kilimo Benki ya Azania, Augustino Matutu, baada ya benki hiyo kuibuka mshindi wa kwanza kwenye taasisi za fedha katika Maonesho ya 7 ya Kitaifa ya Teknolojia ya Madini yaliyofanyika mkoani Geita na kuhitimishwa jana na Rais Samia Suluhu Hassan. Katikati ni Mkuu wa Mkoa wa Geita, Martin Shigela. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Halmashauri yasaka wawekezaji mashambani

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya imetenga mashamba yenye ukubwa wa zaidi ya ekari 52,000 kwa ajili ya kilimo cha pamoja cha mazao ya biashara kwa lengo la kuongeza uzalishaji.

Ofisa Kilimo wa Halmashauri hiyo, Paul Rugodisha aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha kutathmini maandalizi ya msimu mpya wa kilimo unaotarajiwa kuanza mwezi ujao.

Rugodisha, alisema mashamba hayo yametengwa katika vijiji vya Nkung'ungu, Lualaje na Mapogoro ambayo yanayofaa kwa kilimo.

Alisema walitenga mashamba hayo baada ya serikali kuanzisha mpango wa kuwawezesha wanawake na vijana kupitia programu ijulikanayo kwa jina la 'Jenga Kesho iliyo bora' (BBT) ambao Chunya ni miongoni mwa wilaya zitakazonufaika.

Alisema halmashauri hiyo inashirikiana na Wizara ya Kilimo kuandaa mashamba hayo na kugawa kwa wakulima kwa ajili ya kuzalisha mazao mbalimbali.

"Tumeanza na Shamba la Kijiji cha Mapogoro ambalo lina ekari 27,000, tayari limeshakatiwa hatimiliki ambayo ni ya pamoja kati ya halmashauri yetu na wizara na tayari afya ya udongo imepimwa, sasa tunasubiri kuanza kuwapatia wakulima," alisema Rugodisha.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mbaraka Batenga, aliwataka wawekezaji kwenda kuwekeza kwenye kilimo katika wilaya hiyo kwa kuwa wameandaliwa mazingira mazuri ya uwekezaji.

Alisema hali ya hewa ya wilaya hiyo inaruhusu kuzalisha mazao ya chakula na biashara, hivyo wanatakiwa kuchangamkia kuwekeza.

Alisema Chunya ni miongoni mwa wilaya zinazoongoza kwa uzalishaji wa Tumbaku na inashika nafasi ya tatu hali ambayo imeifanya kuunda Mkoa wa Kitumbaku.

"Sisi huku kila zao linakubali tunazalisha tumbaku, tunazalisha mahindi, maharage, karanga, ufuta na mazao mengine mengi, kwa hiyo mtu yeyote anayekuja kuwekeza huku asiogope aje tutamsaidia," alisema Batenga.

Alisema wilaya hiyo pia inazalisha dhahabu kwa kiasi kikubwa na kuwataka wawekezaji kuwekeza kwenye uchimbaji wa madini hayo.

## Wanafunzi wasongamana vyooni

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SHULE ya Sekondari Juhudi Usongwe iliyoko Halmashauri ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi mkoani hapa, inakabiliwa na upungufu wa matundu 22 ya vyoo na kuhatarisha afya za wanafunzi hasa wa kike kutokana na msongamano wakati wa kujisaidia.

Mkuu wa Shule hiyo, Victoria Somola alitoa taarifa hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa mahafali ya kwanza ya kidato cha nne.

Somola, aliwaomba wadau kusaidia ujenzi wa matundu mengine manane ili kukabiliana na changamoto hiyo. Alisema shule hiyo ilijengwa kwa nguvu za wananchi miaka minne iliyopita ina zaidi ya wanafunzi 1,000.

Diwani wa Kata ya Utengule-Usongwe, Yona Ntunjilwa, alisema shule hiyo ilikuwa inakabiliwa na tatizo la utoro wa wanafunzi kutokana na kukosa uzio. Ntunjilwa, alisema tatizo hilo limetatuliwa baada ya shule hiyo kujengewa uzio na kuwadhibiti wanafunzi kutoka wakati wa masomo.

Alisema kwa sasa wanaendelea kutatua kero nyingine shuleni hapo ikiwamo kujenga vyumba vipya vya madarasa ili kukabiliana na msongamano wa wanafunzi na jengo la utawala.

Alisema shule hiyo ilijengwa kwa nguvu za wananchi na baadaye serikali kuwaunga mkono na kwamba wanaendelea kuwaomba wadau kuendelea kushirikiana na wananchi kujenga miundombinu mingine inayohitajika shuleni hapo.

Mgeni rasmi katika mahafali hayo, Mbunge wa Mbeya Vijijini, Oran Njeza, aliiomba halmashauri hiyo kutatua kero zinazoikabili shule ikiwamo ujenzi wa vyoo.





# 46,900 waanza mtihani wa darasa la saba leo

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WANAFUNZI 46,926 visiwani hapa wanatarajia kuanza kufanya mtihani wa taifa wa kuhitimu darasa la saba leo.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Lela Muhammed Mussa, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Lela alisema kuwa kati ya wanafunzi hao watakaofanya mtihani huo, 22,383 ni wavulana sawa na asilimia 47.7 na wasichana 24,543 asilimia 52.3.

**Wanafunzi hao waliosajiliwa kufanya mtihani huo, 30,918 ni wavulana sawa na asilimia 50.6 na 30,125 wasichana asilimia 49.4 .**

Vilevile, alisema wanafunzi 61,043 nao wanatarajia kufanya mtihani wa taifa wa darasa la nne kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba 1, mwaka huu.

Alisema wanafunzi hao waliosajiliwa kufanya mtihani huo, 30,918 ni wavulana sawa na asilimia 50.6 na 30,125 wasichana asilimia 49.4 .

Lela, alisema wanafunzi 23,556 wa kidato cha pili watafanya mtihani wao wa taifa kuanzia Oktoba 30 hadi Novemba 1, mwaka huu.

Kwa mujibu wa waziri huyo, 12,076 ni wavulana asilimia 51.3 na wasichana 11,480 asilimia 48.7.

Alisema kwa upande wa wanafunzi wenye mahitaji malum, 513 wamesajiliwa kufanya mtihani wa darasa la nne 240, la saba 206 na kidato cha pili 67.

"Wizara imejipanga kuhakikisha watu wenye ulemavu wa aina yoyote nao wanapata nafasi ya kufanya mitihani yao kwa mujibu wa miongozo na sera ya serikali," alisema Lela.

Aisisitiza kuwa wizara hiyo imejipanga kuhakikisha mitihani hiyo inafanyika kama ilivyopangwa na kuzitaka kamati za wilaya, walimu na wazazi kushirikiana ili kufikia lengo.




Wadau wa kupinga rushwa ya ngono wakiwamo madereva wa bodaboda wakipita kwenye mitaa ya Bunju A, Dar es Salaam jana, walipokuwa wakiadhimisha Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike na kuhamasisha wananchi kujiandikisha kwa ajili ya uchaguzi wa serikali za mitaa. Maadhimisho hayo yaliandaliwa na Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI). **PICHA: SABATO KASIKA**

# Uhaba wataalamu wa ganzi, usingizi waikabili Zanzibar

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui amesema Zanzibar inakabiliwa na uhaba wa madaktari bingwa wa usingizi na ganzi.

Waziri Mazrui alisema katika kukabiliana na changamoto hiyo nchi inahitaji wataalamu ili kuendana na viwango vya kimataifa.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu Maadhimisho ya Siku ya Ganzi na Usingizi ambayo kila mwaka hufanyika Oktoba 16.

Alisema kwa mwaka huu kauli mbiu hayo ni ganzi na usingizi makini kwa upasuaji salama.

Mazrui, alisema licha ya serikali kuweka miundombinu katika sekta hiyo, bado kuna changamoto ya kupungua kwa wataalamu wa dawa za usingizi na ganzi.

"Mpaka sasa nchi ina watoa huduma ya ganzi na usingizi 49 Unguja na Pemba, licha ya kuwapo kwa vituo vya afya vya umma," alisema.

Aliwaomba wasomi kuchukua kada hiyo ili kuwasaidia wagonjwakupata huduma bora ya upasuaji na usio na madhara.

Aliwataka wasomi wa kada za utabibu kwenda kusomea masomo ya ganzi na usingizi ili kupata wauguzi bora katika vipo vyuo vingi nchini.

Daktari Bingwa wa Ganzi na Usingizi, Mwadini Simai, alisema serikali imeweka vitendea kazi muhimu ikiwamo dawa za kutosha baada ya upasuaji kwa wagonjwa.

Aliwataka wataalamu kuendelea kujengeana uwezo ili kujenga taifa lenye wataalamu bora na kuimarisha afya bora kwa wananchi visiwani hapa.

# Njia mtoto wa kike kujinasua kwenye unyanyasaji yatajwa

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul, amesema njia pekee ya mtoto wa kike kuepuka unyanyasaji ni kusoma kwa bidii na kufikia malengo.

Anna, aliyasema hayo katika Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Mtoto wa Kike iliyofanyika Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) Kampasi ya Maruhubi kisiwani Unguja.

Alisema watoto wa kike wakisoma kwa bidii itasaidia kutimiza malengo yao ya baadaye na kujiepusha na vitendo viovu, ikiwamo unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka jana, matukio 1,954 ya ukatili na udhalilishaji yaliripotiwa kati yao ya wasichana yalikuwa 1,263 sawa na asilimia 77.1.

Waziri huyo, alisema takwimu hizo zinaonesha kuwa bado watoto wa kike wanahitaji kupatiwa elimu kwa nguvu zote ili kuondokana na vitendo hivyo.

Wakizungumza katika maaadhimisho hayo wasichana, akiwamo Fatma Salum wa Shule ya Tumekuja, alisema ni vema wazazi na walezi wakatenga muda maalum wa kuzungumza na watoto ili kuyajua mambo yanayowakwaza katika mazingira yaliyowazunguka.

Mtaalamu wa Elimu wa Shirika la Kusaidia Watoto Duniani Kanda ya Tanzania, Henry Tindwa, alisema wataendelea kusaidia watoto kujielewa ili kupunguza wimbi la udhalilishaji dhidi yao.



**kwa mujibu wa takwimu za Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali kwa mwaka jana, matukio 1,954 ya ukatili na udhalilishaji yaliripotiwa kati yao ya wasichana yalikuwa 1,263 sawa na asilimia 77.1.**

# Askofu: Anayebeza maendeleo nchini amwulize mama yake

**Na Vitus Audax, MWANZA**

ASKOFU Mkuu wa Jimbo Kuu Katoliki Mwanza, Mhashamu Renatus Nkwande, amewataka Watanzania wote kuheshimu hatua za maendeleo yaliyofikiwa na taifa hivi sasa.

Amesema kuwa miaka 60 iliyopita watu walilazimika kwenda Kenya kununua sabuni na dawa ya meno kwa kuwa havikupatikana nchini.

"Mwalimu (Julius) Nyerere alishawahi kusema 'tunakimbia wakati wenzetu wanatembea', hivyo mbio zetu za Mwenge na mbio za maendeleo ndizo zilizotufikisha hapa.

"Tusibeze maendeleo tuliyoyapata kwa sasa, bila shaka wale wanaoweza kubeza leo waende wakawaulize mama zao," alisema.

Askofu Nkwande alisema hayo mapema jana wakati wa ibada ya kumwombea Hayati Mwalimu Nyerere iliyofanyika katika Parokia ya Mt. Fransisco wa Exavery Nyakahoja, jijini Mwanza.

Ibada hiyo ilihudhuriwa na Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais Dk. Philip Mpango, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa pamoja na viongozi wengine wengi wa serikali na vyama vya kisiasa.

"Miaka 60 iliyopita maisha hayakuwa kama ya leo, hata miaka 50 ninayoifahamu mimi tofauti ipo, kuna wakati mimi niliishi Musoma miaka fulani, baada ya vita maisha tuliyokuwa nayo yalikuwa magumu, ya ovyo na wakati mwingine tulivuka ng'ambo kwenda Kenya ili tukanunue mche wa sabuni, dawa ya meno, hapa kwetu hapakuwa na kitu.

"Tulikuwa tunavaa lakini hatufui kwa sabuni, tulitumia majani ya mipapai na hata wakati mwingine mizizi kufulia nguo na sisi tuliokwenda shuleni, tulitumia kipande kimoja cha sabuni kufulia na kuogea kwa miezi sita halafu unasema hatujaendelea! Kamwulize mama yako, atakuhadithia jinsi maisha yalivyokuwa," alisema Askofu Nkwande. Alisema kuwa kwa miaka yote hiyo nchi imefika ilipo kwa juhudi za Watanzania wenyewe pamoja na viongozi walioongoza, hivyo hakuna budi kuwapenda na kuthamini mchango wao.

Alisema kwa sasa ni zamu ya Rais Samia, hivyo kumtaka apeleke taifa katika hatua nyingine na kumshukuru kwa mazuri aliyoyafanya hadi sasa na kuendelea kuyafanyia kazi yale waliyoyaacha watangulizi wake. Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na Uchaguzi Mkuu, Askofu Nkwande aliwataka Watanzania kushiriki kwa hekima na busara na si kupambania madaraka.

"Huwa ninajiuliza hivi 'na mimi nisingekuwa padri ningegombania jinsi hii?' Unakuta mtu anakamia na mishipa inamtoka, anataka awe mbunge, anadiriki hata ampige mwenzake, hatujafika huku kama walipofikia wengine huko.

"Lakini dalili tunaziona na hata tunazisikia, inasikitisha hapa tulipo ni pazuri, lakini msifanye huko tunakoelekea kukawa kubaya zaidi," alisisitiza Askofu Nkwande.

Akizungumza kwa niaba ya Rais Samia, Makamu wa Rais, Dk. Mpango, alisema dhumuni la kufanya ibada hiyo ni kumwombea Baba wa Taifa ili hata Rais pamoja na wasaidizi wake wajaliwe hekima ya kuwatumikia Watanzania.

"Baba wa Taifa aliongoza kwa ustadi katika kuwaunganisha Watanzania na kuzifanya kabila zaidi ya 120 na kuwa kitu kimoja sambamba na kutuunganisha kwa lugha moja ya Kiswahili," alisema Dk. Mpango.




Waziri wa Afya, Jenista Mhagama (kulia), akimpa tuzo Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya Ocean Road, Dk. Julius Mwaiselage, kwa kufanya vizuri kwenye tiba ya saratani wakati wa kuzindua Kituo cha Tiba na Utafiti wa Saratani Shifaa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Mwenge wa Uhuru wazindua shule yenye thamani ya milioni 540/-

**Na Mwandishi Wetu, MAGU**

MWENGE wa Uhuru umezindua mradi wa ujenzi wa Shule mpya ya Msingi Igudija uliogharimu Sh. milioni 540.3, fedha kutoka Serikali Kuu kupitia Programu ya BOOST.

Mradi huo unajumuisha ujenzi wa vyumba vya madarasa 16, matundu ya vyoo 24, jengo la utawala, utengenezaji madawati 210, meza 30 za elimu ya awali pamoja na viti vyake 30, viti vya walimu 14 na meza 17.

Mradi huo ulioko katika kata ya Kisesa, wilayani Magu mkoani Mwanza, ulitekelezwa kwa kutumia utaratibu wa 'Force Account' na kukamilika kwa asilimia 100 na unaendelea kutoa huduma.

Shule hiyo ilizinduliwa na Kiongozi wa Mbio za Mwenge Kitaifa, Godfrey Mzava mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Magu, Joshua Nassari na viongozi wengine wa halmashauri waliohudhuria.

Mkuu wa Shule hiyo, Benifaxad Chiguru alisema kukamilika kwa mradi huo kumesaidia kupunguza msongamano wa wanafunzi katika shule za Kisesa, Muungano, Wita, Igekemaja na Kitumba.

Mmoja wa wananchi wenye watoto wanaosoma katika shule hiyo, Prisca Revocatus alishukuru serikali kwa ujenzi wa shule hiyo ambao umeondoa changamoto ya watoto kutembea umbali mrefu kwenda Shule ya Msingi Kisesa na kuwaepusha na ajali zilizosababishwa na kuvuka barabara.

Mwenyekiti wa Kamati ya shule, Abel Elikana, alisema ujenzi huo utapunguza pia ajali za barabarani kwa kuwa watoto kwa sasa hawavuki barabara kwenda upande wa pili kufuata huduma ya elimu huku miti 800 ikipandwa kuzunguka eneo la shule ili kuhakikisha mazingira yanatunzwa.

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa, Mzava, alisema Rais Samia Suluhu Hassan anawapenda wananchi wake na anaendelelea kuamini kuwa urithi wa mtoto ni elimu, ndio maana akaridhia kutolewa fedha hizo kwa kuwajengea shule mpya ya awali na msingi katika kijiji cha Idugija badala ya kuchangisha wananchi.

## Wachimbaji madini walia utitiri wa kodi

**Na Thobias Mwanakatwe, SONGWE**

WACHIMBAJI madini katika mikoa ya Songwe na Mbeya wamesema utitiri wa kodi na tozo wanazotozwa na serikali, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), halmashauri na taasisi nyingine za serikali umekuwa kichocheo kinachowafanya wachukue uamuzi mgumu kutorosha dhahabu na kwenda kuuza kinyemela.

Walisema hayo jana mbele ya Mkuu wa Wilaya ya Songwe, Solomon Itunda, wakati wa maonesho ya wachimbaji madini yaliyofanyika kata ya Saza, wilayani humo.

Maonesho hayo ambayo ni ya kwanza kufanyika wilayani na mkoani Songwe yakiwashirikisha wachimbaji wadogo wa kati na wakubwa, yana lengo la wachimbaji kubadilishana mawazo na uzoefu wa namna ya kufanya kazi za uchimbaji.

Meneja Mkuu wa Kampuni ya Songwe Gold Family (SGF), Michael Matoke, alisema kuna tozo na kodi za malimbikizo ya madeni ya nyuma ambayo serikali ilitangaza kuyasamehe, lakini TRA inaendelea kuwatoza wachimbaji, hali inayowafanya washindwe kujua msimamo wa serikali.

"Suala hili la tozo za malimbikizo ya madeni ya nyuma kwa namna moja au nyingine linachangia hata utoroshaji dhahabu kwa sababu wachimbaji wengine hawana hata mitaji, sasa unapompigia mahesabu ya nyuma wakati kwenye akaunti yake hana hata Sh. milioni 20, huyu unamfanya awaze zaidi," alisema.

Matoke ambaye alizungumza kwa niaba ya wachimbaji, alisema ili kuondoa mkanganyiko uliopo, uongozi wa serikali ya wilaya uingilie kati jambo hilo na kulifikisha katika ngazi za juu za serikali lipatiwe ufumbuzi kwa kuwa linawaumiza vichwa wachimbaji.

Kuhusu tozo ya asilimia mbili wanayotozwa na TRA kila wanapouza madini, alisema ni kubwa, serikali iangalie uwezekano wa kuipunguza na kufikia asilimia moja kwa kuwa mbali na kodi hiyo, zipo nyingine kama asilimia saba wanazotozwa na hivyo kufanya mchimbaji kutozwa jumla asilimia tisa za kodi.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya **DODOMA MJINI**
Kituo cha MJINI **Mkoa DODOMA**
Shauri la Madai/Ndoa Na 118/2024
Jina la mdai **BOAZ CHARLES ISANZU**
Jina la Mdaiwa **FAITH MWENAWA MWIKALI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa FAITH MWENAWA MWIKALI**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai)**
**MADAI YA TALAKA KUACHANA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 16 Mwezi 10 Mwaka 2024 saa 2:30 asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama itaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.**

**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 11 Mwezi 10 Mwaka 2024**

HAKIMU
URBAN COURT
PRINCIPAL PRIMARY COURT MAGISTRATE URBAN DODOMA

**TANGAZO KUPOTEA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA**

**EDRICK EMILIANO NANYARO** anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki wa kiwanja Na 393 Kitalu "MM"kilichopo Bushushu Manispaa ya Shinyanga

Atakaeiona nyaraka hiyo atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

Taarifa ya polisi
**PHQ/SHI/SHI/9145/2024**

# DRC, Rwanda watia saini makubaliano ya kiusalama

**KINSHASA, DRC**

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) na Rwanda wametia saini juu ya mpango wa usalama wa mashariki mwa DRC ambao unaweza kusababisha kuondolewa kwa maelfu ya wanajeshi wanaoaminika kupelekwa katika eneo hilo na Kigali.

Taarifa kuhusu makubaliano hayo lilitolewa na serikali ya Angola, ambayo ni mpatanishi wa Umoja wa Afrika (AU) wa mzozo wa mashariki mwa DRC, licha ya kwamba uthibitisho rasmi bado haujatolewa na nchi hizo mbili.

Taarifa hiyo ilisema mawaziri wa mambo ya nje wa DRC na Rwanda walifikia makubaliano hayo mjini Luanda juu ya mpango ulioainishwa kuwa ni wa kuondoa kundi la waasi wa Kihutu lililoundwa na wahusika wa mauaji ya kimbari ya mwaka 1994.

Ilisema kuwa mpango wa kina utafanyiwa kazi katika mazungumzo yajayo kati ya pande hizo mbili.

Ilielezwa kuwa majaribio ya awali ya kukamilisha makubaliano hayo, ambayo maelezo yake yalitolewa wakati wa mazungumzo ya siri mwezi Agosti kati ya wakuu wa kijasusi wa nchi hizo mbili, yalishindwa kutekelezwa huku kila upande ukitaka upande mwingine utimize wajibu wake kwanza.

Ilibainishwa kuwa wajumbe hao wawili pia walisisitiza umuhimu wa kuheshimu usitishaji mapigano ulioyumba kati ya vikosi vya serikali na waasi wa M23 wanaotawaliwa na Watutsi.

Katika hatua nyingine, Rais wa RDC Félix Tshisekedi alithibitisha kuhusu kuendelea kwa ushirikiano wa kijeshi kati ya jeshi la Kongo na Uganda katika mapambano dhidi ya waasi wa ADF katika mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri.

Uamuzi huo ulithibitishwa baada ya mkutano wa kutathmini operesheni katika mji mkuu wa Kongo kuanzia Oktoba 10 hadi 11, mwaka huu kati ya wakuu wa majeshi ya DRC na Uganda.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ofisi ya rais wa DRC kupitia X, mkuu huyo wa nchi alitoa maelekezo ya wazi ya kuimarishwa kwa ushirikiano wa kijeshi kati ya DRC na Uganda ili kutokomeza ukosefu wa usalama katika mikoa ya Kivu Kaskazini na Ituri.

Taarifa ya kuendelea kwa ushirikiano huu wa kijeshi inakuja huku Uganda ikilaumiwa na mashirika ya kiraia kwa kuwaunga mkono waasi wa M23.

Ilielezwa kuwa operesheni za pamoja kati ya jeshi la Kongo na Uganda zilianzishwa Novemba 30, 2021 dhidi ya ADF.

Hata hivyo, ilielezwa kuwa Agosti, mwaka huu mashirika ya kiraia katika mikoa ya Ituri, Kivu Kaskazini na Kusini yaliiomba serikali ya DRC kufafanua uhusiano wa kidiplomasia na Uganda, ambayo pia inawaunga mkono waasi wa M23, wanaoungwa mkono pia na Rwanda.

Ripoti ya hivi punde kutoka kwa wataalamu wa Umoja wa Mataifa (UN) inashutumu Uganda kwa kuuwezesha mkutano wa maofisa wa M23 na AFC nchini Uganda.

Washirika wa karibu wa Jenerali Muhoozi Kainerugaba, kamanda wa vikosi vya Uganda, walinyooshewa kidole katika ripoti hiyo. Huku Jenerali Kainerugaba, katika taarifa zake kwenye ukurasa wake wa X, hafichi kuunga mkono M23.

*RFI*



Wauguzi wakimhudumia mmoja wa raia wa Kipalestina waliojeruhiwa katika shambulio la Israel lililolenga Shule ya Al Muft iliyoko Ukanda wa Gaza, ambalo pia limesababisha vifo 15 na majeruhi 50, jana. **PICHA: MTANDAO**

# Russia yadaiwa kuwaua wafungwa Ukraine

**MOSCOW, Russia**

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa Ukraine, Andrii Sybiha, ametoa wito wa msaada kutoka kwa jamii ya kimataifa kutokana na ripoti za madai kwamba wanajeshi wa Russia wamewapiga risasi wafungwa wa kivita wa Ukraine.

Katika ujumbe uliotolewa kupitia mtandao wa kijamii wa X jana, Sybiha alisema kuwa Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (ICC) lazima itoe hati za kukamatwa kwa wale aliowaita wauaji na watesaji wa Russia.

Sybiha pia alitoa wito kwa waangalizi wa kimataifa na madaktari kupewa idhini ya kufikia kambi za wafungwa, na kwamba Umoja wa Mataifa unaamini kuwa asilimia 95 ya wanajeshi wa Ukraine waliotekwa na Russia wanakabiliwa na mateso.

Matamshi ya Sybiha yanakuja baada ya ripoti za kuuawa kwa wanajeshi tisa wa Ukraine waliokuwa wamejisalimisha wakati wa mapigano katika eneo la Kursk magharibi mwa Russia baada ya kutumia risasi zao zote.

Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya Ukraine, wanajeshi hao waliuawa papo hapo.

Kamishna wa Haki za Kibinadamu wa Ukraine, Dmytro Lubinets, alihimiza Umoja wa Mataifa na Kamati ya Kimataifa ya Msalaba Mwekundu kuchukua hatua.

Katika ujumbe mwingine uliotolewa kupitia mtandao wa kijamii wa X, Lubinets alisema, Russia ni taifa la kigaidi linalokiuka sheria zote za vita, na kwamba jamii ya kimataifa haipaswi kupuuza uhalifu kama huo.

Ilielezwa kuwa siku chache zilizopita, mwanajeshi mmoja wa Russia alikamatwa kwa madai ya kuwapiga risasi wanajeshi kadhaa wa Ukraine akiwa na wenzake baada ya wanajeshi hao kujisalimisha.

Ofisi ya mwendesha mashtaka mjini Kiev, imesema inahafamu kuhusu zaidi ya visa 90 vya mauaji ya wafungwa wa kivita wa Ukraine.

*DW*

# Mashambulizi ya Hezbollah yatikisa Israel

**BEIRUT, Lebanon**

MASHAMBULIZI ya droni ya Hezbollah yameua wanajeshi wanne wa Israel na kujeruhi zaidi ya watu 60 katika kambi ya jeshi karibu na Haifa, huku Jerusalem ikijibu kwa mashambulizi ya anga na mapigano makali yakiendelea mpakani na Gaza.

Ilielezwa kuwa shambulizi hilo lilifanyika kwenye kambi ya mafunzo ya kijeshi huko Binyamina, karibu na Haifa, likiwa shambulizi la vifo vingi zaidi dhidi ya kambi ya jeshi tangu Septemba 23, wakati Israel ilipoongeza mashambulizi yake dhidi ya Hezbollah nchini Lebanon.

Hezbollah ilidai kuhusika na shambulizi hilo la droni, ikisema kuwa ilikuwa ni kulipiza kisasi mashambulizi ya anga ya Israel, yakiwamo yale yaliyofanyika Alhamisi, ambapo Wizara ya Afya ya Lebanon iliripoti kuwa watu wasiopungua 22 walipoteza maisha katikati mwa Beirut.

Huku mashambulizi ya pande zote yakiendelea, vikosi vya Israel vilifanya mashambulizi ya anga kwenye vituo vya Hezbollah vya kurusha roketi kwenye vituo vya silaha, na maeneo mengine ya kimkakati. Pia ilielezwa kuwa vikosi vya Hezbollah vilikabiliana na wanajeshi wa Israel waliokuwa wakijaribu kuingia kwenye vijiji vilivyo karibu na mpaka.

Katika hatua nyingine Umoja wa Mataifa ulitoa ripoti ya ukiukaji wa amani, ukidai kuwa wanajeshi wa Israel waliingia kwa nguvu kwenye moja ya vituo vya walinda amani vya UNIFIL nchini Lebanon.

Wakati huo huo, mashambulizi ya Israel yameendelea huko Gaza na kusababisha vifo vya raia, wakiwamo watoto na familia nzima katika shule moja iliyotumiwa kama kimbilio, huku jumla ya watu 15 wakiuawa na wengine zaidi ya 50 wamejeruhiwa.

Ilielezwa kuwa mgogoro huo unaendelea kusababisha hasara kubwa kwa pande zote, huku dunia ikiendelea kutoa wito wa amani na utulivu katika eneo hilo.

*DW*

# KINARA WA MABAO LIGI KUU MCHEZAJI BORA SEPTEMBA

**Na Adam Fungamwango**

KINARA wa ufungaji mabao Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka kufikia raundi ya saba msimu huu, Selemani Mwalimu wa Fountain Gate FC, amechaguliwa kuwa mchezaji bora wa Septemba, huku kocha wa timu hiyo, Mohamed Muya, naye akitangazwa kuwa bora kwa mwezi huo.

Taarifa iliyotolewa jana na Bodi ya Ligi nchini (TPLB), ilieleza kuwa washindi hao wote wamechaguliwa na Kamati ya Tuzo ya Shirikisho la Mpira wa Miguu (TFF), huku tuzo pia ikienda kwa Godwin Israel ambaye ameshinda nafasi ya meneja bora, akiwa anahudumu kwenye Uwanja wa Tanzanite Kwaraa, uliopo Babati mkoani Manyara.

„Mwalimu alionesha kiwango kizuri chenye mwendelezo kwa mwezi huo, akiwashinda Edgar William wa Fountain Gate na Feisal Salum wa Azam FC ambao aliingia nao fainali katika mchakato huo.

„Muya aliwashinda Rachid Taoussi wa Azam FC na Denis Kitambi wa Singida Black Stars," ilisema sehemu ya taarifa hiyo.

Katika mwezi huo, Fountain Gate ilishinda mabao 2-1 dhidi ya KenGold, ikashinda tena 3-1 dhidi ya Tabora United, idadi kama hiyo ya ushindi dhidi ya Kagera Sugar, ikitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Dodoma Jiji, hivyo kupaa kutoka nafasi ya 15 hadi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu, ingawa kwa sasa imeshuka hadi nafasi ya tatu, ikipigwa kumbo na Simba.

Mwalimu, amepachika mabao matano mpaka sasa na yupo juu ya orodha ya wafungaji bora wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Wakati huo huo, kamati hiyo pia imemchagua straika wa Mtibwa Sugar, Raizin Hafidh kuwa mchezaji bora wa mwezi kwa Ligi ya Championship.

Mchezaji huyo anayeongoza kwenye ufungaji bora akiwa na mabao manne, Septemba alipachika matatu, huku kocha wa timu hiyo, Melis Medo, akichaguliwa kuwa kocha bora, akiwashinda Abdul Mingange wa Stand United na Mussa Omar wa Biashara United.

MILIKI...



Mchezaji wa Timu ya Chuo cha Kampala, Evans Mwakyenda, akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa Boa, Shaban Ramadhan, katika mchezo wa kirafiki uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mbeya City, TMA zatakata Championship

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City na TMA, zimepata ushindi katika michezo yao ya raundi ya nne ya Ligi ya Championship, inayoendelea nchini kusaka timu zitakazopanda Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Mbeya City ikiwa ugenini Uwanja wa Highland Park, Morogoro juzi, iliishindilia African Sports mabao 3-1, huku TMA nayo ikipata ushindi kama huo nyumbani, Sheikh Amri Abeid, ikicheza dhidi ya Stand United.

Mabao ya Mbeya City yalifungwa na Malack Joseph dakika ya 19, kabla ya straika wao tegemeo na wa siku nyingi, Eliud Ambokile kufunga mawili, dakika ya 48 na 83, Ali Baluba akifunga la kufutia machozi dakika kumi kabla ya mchezo kumalizika.

African Sports, yenye maskani yake mjini Tanga, inautumia uwanja huo kutokana na Mkwakwani kuwa kwenye matengenezo.

Matokeo hayo yanaifanya Mbeya City kukwea hadi nafasi ya nne ikiwa na pointi saba, huku African Sports, ikibaki na pointi yake moja katika nafasi ya 13 ya msimamo wa ligi hiyo.

TMA ilikwea hadi nafasi ya pili kutokana na ushindi huo wa mabao 3-1 dhidi ya Stand United, kwa mabao yaliyowekwa wavuni na Ramadhani Kapera aliyefunga mawili na Abdulaziz Shahame aliyefunga moja.

Timu hiyo imefikisha pointi 10, ikiwa nyuma ya vinara, Mtibwa Sugar, ambayo ina pointi 12 mpaka sasa, huku Stand United ikibaki na pointi zake tisa, ikiwa nafasi ya nne, nyuma ya Songea United yenye pointi kama hizo, lakini inakamata nafasi ya tatu kwa tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

# Mlandege FC yapinga kupiga 'bomu mochwari'

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU ya Mlandege FC imesema haijapiga bomu mochwari (haijakutana na kibonde), bali ilistahili kushinda kwa idadi kubwa ya mabao kutokana na viwango vikubwa walivyoonesha wachezaji wake juzi, Jumamosi.

Mlandege FC juzi, iliibuka na ushindi mnono wa mabao 10-0 dhidi ya Inter Zanzibar FC katika mwendelezo wa Ligi Kuu Zanzibar mzunguko wa sita, mchezo huo ukichezwa katika Dimba la New Amaan Complex, visiwani hapa.

Timu ya Inter Zanzibar FC ni miongoni mwa timu tatu ambazo hazijawahi kushinda katika michezo yake ya Ligi Kuu Zanzibar ambapo ina alama moja.

Kwa matokeo hayo, Mlandege FC imepanda hadi nafasi ya tatu ikiwa na alama 12, sawa na Malindi SC ambayo ipo nafasi ya nne na Mwembe Makumbi City iliyoko nafasi ya tano.

Akizungumza na gazeti hili baada ya mechi hiyo, Kocha wa Mlandege FC, Hassan Ramadhani, alisema ni furaha ya kila timu kuona inapata ushindi mkubwa katika ligi ngumu hasa Ligi Kuu Zanzibar.

Alisema ushindi wa mabao hayo haimaanishi kama wapinzani wao ni wabovu kwani hawajawahi kuamini kwamba Ligi Kuu Zanzibar kuna timu mbovu.

Kocha huyo alisema ushindi huo umetokana na maboresho makubwa aliyoyafanya ndani ya kikosi chake baada ya kuambulia sare katika mchezo uliopita kabla ya huo wa juzi.

Aidha, alisema kwa sasa hana hofu na timu yake kwa kila mchezo ambao atashuka uwanjani anatarajia kupata matokeo mazuri.

"Tumepata matokeo haya kwa kuwa tumewazidi ujanja wapinzani wetu, ila hakuna timu mbovu katika Ligi Kuu, timu zote ni nzuri bali tunatofautiana kwa viwango vya wachezaji.

Kwingineko katika matokeo mengine ya ligi hiyo, timu ya Malindi SC nayo iliondoka uwanjani na alama tatu baada ya kuwalaza New City kwa mabao 2-1, kwenye mchezo uliochezwa katika Uwanja wa Mau A.

## ZISIKUPITE

### SALIBA KUBAKIZWA

ARSENAL wana imani kuwa mlinzi wa Ufaransa, William Saliba mwenye umri wa miaka 23, atasalia katika Uwanja wa Emirates licha ya Real Madrid kumtaka. ***(Express)***

### COLVERT-LEWIN NA JUVE

KLABU ya Juventus inaweza kumnunua mshambuliaji wa Everton, Dominic Calvert-Lewin mwenye umri wa miaka 27, ambaye mkataba wake utamalizika msimu wa majira ya joto. ***(Corriere dello Sporti)***

### HOENESS KAIKATAA UNITED

MANCHESTER United walimtaka Kocha wa Stuttgart, Sebastian Hoeness mwenye umri wa miaka 42, kuchukua nafasi ya Erik ten Hag msimu uliopita, lakini akawakataa. ***(Bild)***

### TUCHEL AHUSISHWA

MANCHESTER United bado iko kwenye nafasi ya kumsajili kocha wa zamani wa Chelsea na Bayern Munich, Thomas Tuchel, licha ya kocha huyo mwenye umri wa miaka 51, kuhusishwa na kibarua cha Timu ya Taifa ya England. ***(TeamTalks)***

### PENDERS HUYOOO CHELSEA

CHELSEA ilijiweka kifua mbele msimu uliopita ilipoishinda Bayern Munich katika kuinasa saini ya mlinda lango wa Genk, Mike Penders mwenye umri wa miaka 19 raia wa Ubelgiji, ambaye atahamia Stamford Bridge Julai ijayo. ***(Fabrizio Romano)***

### OYEDEJI AWINDWA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Nathan Butler-Oyedeji mwenye umri wa miaka 21, anawindwa na Borussia Monchengladbach. ***(Football Insider)***

### FRIEDRICH KUONDOKA JANUARI

MLINZI wa Kati wa Ujerumani, Marvin Friedrich mwenye umri wa miaka 28, anaweza kuondoka Borussia Monchengladbach Januari. ***(Sky Sport Germany)***

### SUDAKOV AGOMBEWA

ARSENAL imeungana na Tottenham Hotspur katika kinyang'anyiro cha kumsajili kiungo mshambuliaji wa Ukraine, Georgi Sudakov mwenye umri wa miaka 22, kutoka Shakhtar Donetsk. ***(Caught Offside)***

### SANE KWA BARCA, ARSENAL

BARCELONA, Arsenal na Newcastle United zote zina nia ya kumsajili winga wa Ujerumani, Leroy Sane mwenye umri wa miaka 28, kutoka Bayern Munich**. *(Ekrem Konur)***

### DIBLING ASHAWISHIWA

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionesha nia ya kutaka kumnunua. ***(GiveMeSport)***

### CONNOLLY AWANIWA

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ODEGAARD KUREJEA MAPEMA DIMBANI

●●●Arsenal hawajaweka muda rasmi, lakini nahodha huyo anatarajiwa ifikapo...

**LONDON, England**

MARTIN Odegaard huenda akarejea dimbani mapema zaidi tofauti na ilivyofikiriwa mwanzo, kwa mujibu wa Sky Sport.

Nahodha huyo wa Arsenal aliachwa katika mapumziko ya kimataifa ya Septemba, na ingawa 'Washikabunduki' hao hawajaweka muda rasmi wa kupona kwake, inatarajiwa kwamba Odegaard atakuwa fiti vya kutosha kurejea dimbani Novemba.

Katika kipindi cha sasa cha mapumziko ya kimataifa, ripoti zilibuka kwenye mitandao ya kijamii zikidai Odegaard alikuwa amepatwa na tatizo ambalo sasa lilimfanya akabaliane na kurejea ama Desemba au mapema 2025.

Lakini Sky Sports News ieleza kwamba, Odegaard anaendelea kupona haraka na atakuwa dimbani Novemba.

Hivi majuzi Arsenal ilishiriki video ya Odegaard akikimbia kwenye kinu cha kukandamiza nguvu ya uvutano - ishara kwamba bado hajaridhika kuweka uzito wake kamili kwenye kifundo cha mguu wake - huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway akielezea uzoefu huo kama „usio halisi".

Huku Odegaard akiendelea kuimarika, Arsenal sasa inavuja jasho kutokana na utimamu wa winga Bukayo Saka, ambaye alijiondoa kwenye kikosi cha England Jumamosi baada ya kupata jeraha kwenye kichapo kutoka kwa Ugiriki.

Ukubwa wa jeraha lake bado haujajulikana.

# Hoeness akataa kumrithi Ten Hag

**MANCHESTER, England**

KLABU ya Manchester United ilikataliwa mpango wake wa kutaka kumchukua kocha wa Stuttgart, Sebastian Hoeness, wakati wa majira ya joto kabla ya kuamua kumbakisha Erik ten Hag, ripoti ya ESPN imefichua.

Baada ya kampeni ya kusikitisha ya 2023/24, Ten Hag aliingia msimu wa majira ya joto chini ya shinikizo kubwa chini ya wamiliki wapya Sir Jim Ratcliffe na INEOS waliofanya ukaguzi wa utenda kazi wake baada ya msimu.

Mawasiliano yalifanywa na wasimamizi wachache, akiwamo Thomas Tuchel, huku maofisa wa United wakitafuta kujua kama Ten Hag ndiye bosi bora zaidi wakati huo.

Kwa mujibu wa gazeti la Bild, kocha mwingine aliyewasiliana na United ni Hoeness wa Stuttgart, ambaye hisa zake zilipanda hadi viwango vipya msimu uliopita wakati timu yake ilipomaliza nafasi ya pili kwenye Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, mbele ya Bayern Munich na nyuma ya Bayer Leverkusen.

Inadaiwa kuwa United iliwasiliana na Hoeness ili kujadili uwezekano wa kuhamia Old Trafford, lakini kocha huyo mwenye umri wa miaka 42, ambaye alihusishwa na Chelsea majira ya kiangazi, alikataa.

Hoeness alifurahishwa na mbinu ya United, lakini alihisi kazi yake huko Stuttgart bado haijakamilika na akakataa nafasi hiyo.

United hatimaye waliamua kumpa Ten Hag nyongeza ya mkataba, lakini kwa mara nyingine wakajikuta wakilazimika kufanya chaguo kuhusu mustakabali wake wiki hii.

Viongozi wa klabu walikutana katika mkutano uliopangwa na kuongeza utendaji duni wa Ten Hag kwenye ajenda, na hatimaye kuamua kuendelea na Mholanzi huyo.

# Tchouamen hana mpango na Liverpool

**MADRID, Hispania**

KIUNGO wa kati wa Real Madrid, Aurelien Tchouameni, hana nia ya kuondoka mji mkuu wa Hispania Madrid na Liverpool, kwa mujibu wa ripoti ya magazeti ya Ulaya.

Nyota huyo wa Ufaransa amekosa mchezo mmoja pekee kwa Madrid hadi sasa msimu huu baada ya kupata jeraha lililomfanya akose ushindi wao wa mabao 2-0 dhidi ya Real Sociedad.

Amekuwa sehemu muhimu ya kikosi chao tangu alipowasili msimu wa majira ya joto wa 2022, akiisaidia Madrid kubeba taji la ligi na taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu wa 2023/24.

Hata hivyo, amekuwa akihusishwa na kuhamia Liverpool baada ya 'Wekundu' hao kushindwa kuipata saini yake hapo awali.

Tchouameni amekuwa kwenye rada za kikosi hicho cha Ligi Kuu England tangu siku zake za kuvutia za Monaco - akihamia Madrid badala ya Anfield mwaka 2022.


Lakini inaonekana Mfaransa huyo hana nia ya kuwaacha nyuma mabingwa hao wa Hispania na angependelea kujitolea kwa mustakabali wake chini ya Kocha Carlo Ancelotti.

Kwa mujibu wa mwandishi Matteo Moretto, Tchouameni hataki kujiunga na kikosi cha kocha Arne Slot na angependelea kuendeleza kipindi chake cha kubeba mataji nchini Hispania.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliichezea Madrid mechi 38 msimu uliopita, akisajili mabao matatu na asisti huku timu yake ikifanikiwa kupata mataji manne - taji la LaLiga, taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super Cup na Super ya Hispania.

'Los Blancos' hao wamefurahia mwanzo mzuri wa kampeni ya 2024/25, wakiwa nyuma kidogo tu ya viongozi Barcelona akiwa na alama 21.

Wanatarajiwa kumenyana na Celta Vigo baada ya mapumziko ya kimataifa hapo Jumamosi wiki hii.



# BAYERN MUNICH YAJITOA KWA ALISSON

**MUNICH, Ujerumani**

KLABU ya Bayern Munich haina nia ya kutaka kumnunua mlinda mlango wa Liverpool, Alisson.

Mustakabali wa muda mrefu wa Alisson ndani ya Anfield umekuwa ukitiliwa shaka mara nyingi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, huku Liverpool wakipanga mipango ya kuondoka kwake kwa kumsajili Giorgi Mamadashvili kutoka Valencia mapema mwaka huu.

Wakati klabu za Saudi Arabia zinamtaka Alisson, tetesi zimependekeza Bayern wanaweza kumnunua nyota huyo wa kimataifa wa Brazil huku wakijiandaa na maisha bila Manuel Neuer ambaye atatimiza umri wa miaka 39, mwaka ujao.

Lakini ripoti ya Bayern imepuuza mapendekezo kwamba wanaweza kujaribu kumnasa Alisson kutoka Liverpool na kusisitiza kwamba mlinda mlango huyo si sehemu ya mipango yao.

Badala yake, Bayern hawako tayari kusitisha uhusiano wao na Neuer na wanatazamia kumpa kipa huyo mkongwe mkataba mpya wa miezi 12 ili kuwa naye hadi 2026.

Bado kuna mipango kwa Alexander Nubel hatimaye kumrithi Neuer katika lango la Bayern.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28, alitumia msimu uliopita kwa mkopo akiwa kule Stuttgart.

Nubel atarejea Bayern mwaka 2026, wakati huo mpango ni yeye kumrithi Neuer.

Alisson, kwa upande wake, bado yuko chini ya mkataba na Liverpool hadi 2027, huku Mamadashvili akipanga kutoa ushindani kwa mahali pake pa kuanzia msimu ujao wa majira ya joto.

HABARI MICHEZO

# HAMZA SASA AREJEA RASMI MAZOEZINI SIMBA

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuumia siku chache zilizopita, beki wa kati wa Klabu ya Simba, Abdulrazaq Hamza, jana alianza rasmi mazoezi kujiandaa na mchezo dhidi ya Yanga Oktoba 19, mwaka huu.

Beki huyo aliumia muda mfupi baada ya kuitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa 'Taifa Stars' kinachocheza mechi za kuwania kufuzu fainali za Afrika za mwakani zitakazofanyika Morocco.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema beki huyo anaendelea vizuri na sasa ameanza mazoezi kuelekea mchezo wao wa 'dabi'.

"Habari njema kwa Wanasimba, kijana wetu Hamza (Abdulrazaq) amerejea mazoezini, yupo na wenzake kujiandaa na mchezo wetu unaofuata," alisema Ahmed.

Alisema kurejea kwa nyota huyo ni habari njema kwa benchi la ufundi ambapo watakuwa na kikosi kilichokamilika kuelekea kwenye mchezo wao dhidi ya Yanga.

Ahmed, alisema kocha Fadlu Davids atakuwa na eneo pana la kuchagua kikosi chake kuelekea kwenye mchezo huo utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tunaomba Mungu wachezaji wetu waendelee kuwa kwenye afya nzuri, wasipate majeraha kuelekea kwenye mchezo wetu, tunaamini Wanasimba watafurahi siku hiyo," alisema Ahmed.



Kocha wa Simba, Fadlu Davids, akimpongeza kiungo wa timu hiyo, Jean Charles Ahoua, kwa kumkumbatia baada ya kufunga bao wakati wakishinda 4-0, dhidi ya Fountain Gate, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Agosti, mwaka huu, katika Uwanja wa KMC, Dar es Salaam. Ahoua anapewa nafasi kubwa ya kuibeba timu hiyo kwenye mechi ya 'Dabi' ya Kariakoo, dhidi ya Yanga itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi wiki. **PICHA: MAKTABA YETU**

## Simba kamili kwa dabi, Yanga yalia na muda

INATOKA UK. 24

walio kwenye kikosi cha Taifa Stars ambacho leo kinajitupa, Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Yanga pia imetoa wachezaji kwenye timu zingine za taifa, kama Stephane Aziz Ki, akiwa kikosi cha Burkina Faso, Kennedy Musonda na Clatous Chama, Timu ya Taifa ya Zambia, Khalid Aucho, akiichezea Uganda Cranes, na Djigui Diarra, akiitumikia Timu ya Taifa ya Mali.

Akiizungumzia presha katika mchezo huo kwa viongozi na mashabiki, Harrison alisema ni lazima iwepo kwani dabi ya Simba na Yanga ina hisia kubwa zaidi ya mchezo wenyewe wa soka.

Hata hivyo, alisema kwa viongozi hauwezi kuwapa presha kiasi cha kuzimia kama mashabiki au kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yao.

"Hata sisi viongozi tunakuwa na presha, kwani mechi za dabi ni za kihisia zaidi, huwa zinaenda mbali zaidi ya mchezo wenyewe wa soka, ila kwetu haiwezi kufikia hatua hiyo kama mashabiki kwa sababu unaweza kushindwa hata kutekeleza majukumu yako, hivyo ni lazima tuwe vizuri kwenye utimamu wa akili ili kuhakikisha tunatekeleza majukumu ya klabu, kama vile kuwaandaa vizuri kimwili na kiakili wachezaji, presha yetu haiwezi kuwa sawa na mashabiki," alisema.

Akielezea kama Kocha Mkuu Miguel Gamondi, amebadilisha aina ya mazoezi kuelekea mchezo huo, alisema mazoezi ni yale yale, ila wanachofanya ni kujiweka katika mazingira mazuri zaidi ya kiufundi kuhakikisha wanapata ushindi.

## Stars ni kufa kupona leo

INATOKA UK. 24

okuwapo uwanjani kuwapa hamasa wachezaji ili kuweza kupata ushindi.

"Ni kweli, Waziri Mkuu anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye mchezo wa kesho (leo), tunawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kuwapa hamasa wachezaji kwa sababu ni mchezo muhimu zaidi kwetu, tunahitaji ushindi," alisema Ndimbo.

Kwenye msimamo wa kundi lao, DR Congo wanaongoza kwa kuwa na pointi tisa wakifuatiwa na Stars wenye pointi nne, nafasi ya tatu inashikwa na Guinea wenye pointi tatu huku Ethiopia wakiburuza mkia kwa kuwa kwa pointi yao moja.

Wakati Stars na DR Congo wakiumana leo kwenye mechi yao ya raundi ya nne, Ethiopia na Guinea zitaumana kesho kwenye mchezo wao wa marudiano wa hatua hiyo.

# Dodoma Jiji yaanza kuiwinda Coastal

**Na Ada Fungamwango**

BAADA ya mapumziko ya Kalenda ya FIFA, Dodoma Jiji FC imeanza mazoezi kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union utakaopigwa Ijumaa ijayo Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, uwanja ambao wapinzani wao wameuchagua kuwa wa nyumbani.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Nizar Khalfan, amesema jana kuwa kikosi hicho kimeanza mazoezi kwa kazi moja tu kuhakikisha wanashinda mchezo huo ili kuelekea kwenye malengo waliyojiwekea ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

"Tulipata mapumziko ya siku kama tatu nne hivi, tumerudi kuendelea pale tulipoachia, nakumbuka mechi ya mwisho tulishinda na hii tunakwenda kucheza ugenini dhidi ya Coastal Union kwa hiyo tunajiandaa vizuri.

"Michezo saba tuliyocheza bado haijatuharibia malengo, yako pale pale kuhakikisha msimu ujao tunacheza mechi za kimataifa kwa kushika nafasi nne za juu," alisema.

Katika michezo hiyo, Dodoma Jiji imekusanya pointi tisa, ikishinda miwili, sare tatu na kupoteza miwili, ikikamata nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, alisema wamerejea wakiwa hawana baadhi ya wachezaji ambao ni majeruhi, lakini wanaendelea vizuri na siku mbili tatu watajumuika na wenzao.

"Tuna Ibrahim Ajibu alipata majeraha katika mchezo dhidi ya Simba, halafu kuna nahodha wetu, Hassan Mwaterema naye ni mgonjwa, lakini hawa wote hali zao zinaendelea vizuri, tunaamini mpaka Ijumaa watakuwa wameungana na wenzao, hata kama hawakucheza mechi dhidi ya Coastal Union, basi watacheza mchezo unaofuata dhidi ya JKT Tanzania, Oktoba 29.

Katika mchezo wao wa mwisho kabla ya mapumziko, Dodoma Jiji iliishindilia Tabota United mabao 2-0.

# HAMZA SASA AREJEA RASMI MAZOEZINI SIMBA

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya kuumia siku chache zilizopita, beki wa kati wa Klabu ya Simba, Abdulrazaq Hamza, jana alianza rasmi mazoezi kujiandaa na mchezo dhidi ya Yanga Oktoba 19, mwaka huu.

Beki huyo aliumia muda mfupi baada ya kuitwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ‚Taifa Stars' kinachocheza mechi za kuwania kufuzu fainali za Afrika za mwakani zitakazofanyika Morocco.

Akizungumza na Nipashe jana, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema beki huyo anaendelea vizuri na sasa ameanza mazoezi kuelekea mchezo wao wa ‚dabi'.

"Habari njema kwa Wanasimba, kijana wetu Hamza (Abdulrazaq) amerejea mazoezini, yupo na wenzake kujiandaa na mchezo wetu unaofuata," alisema Ahmed.

Alisema kurejea kwa nyota huyo ni habari njema kwa benchi la ufundi ambapo watakuwa na kikosi kilichokamilika kuelekea kwenye mchezo wao dhidi ya Yanga.

Ahmed, alisema kocha Fadlu Davids atakuwa na eneo pana la kuchagua kikosi chake kuelekea kwenye mchezo huo utakaochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa.

"Tunaomba Mungu wachezaji wetu waendelee kuwa kwenye afya nzuri, wasipate majeraha kuelekea kwenye mchezo wetu, tunaamini Wanasimba watafurahi siku hiyo," alisema Ahmed.



Kocha wa Simba, Fadlu Davids, akimpongeza kiungo wa timu hiyo, Jean Charles Ahoua, kwa kumkumbatia baada ya kufunga bao wakati wakishinda 4-0, dhidi ya Fountain Gate, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Agosti, mwaka huu, katika Uwanja wa KMC, Dar es Salaam. Ahoua anapewa nafasi kubwa ya kuibeba timu hiyo kwenye mechi ya 'Dabi' ya Kariakoo, dhidi ya Yanga itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam Jumamosi wiki. **PICHA: MAKTABA YETU**

# Dodoma Jiji yaanza kuiwinda Coastal

**Na Ada Fungamwango**

BAADA ya mapumziko ya Kalenda ya FIFA, Dodoma Jiji FC imeanza mazoezi kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Coastal Union utakaopigwa Ijumaa ijayo Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, uwanja ambao wapinzani wao wameuchagua kuwa wa nyumbani.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Nizar Khalfan, amesema jana kuwa kikosi hicho kimeanza mazoezi kwa kazi moja tu kuhakikisha wanashinda mchezo huo ili kuelekea kwenye malengo waliyojiwekea ya kucheza mechi za kimataifa msimu ujao.

"Tulipata mapumziko ya siku kama tatu nne hivi, tumerudi kuendelea pale tulipoachia, nakumbuka mechi ya mwisho tulishinda na hii tunakwenda kucheza ugenini dhidi ya Coastal Union kwa hiyo tunajiandaa vizuri.

"Michezo saba tuliyocheza bado haijatuharibia malengo, yako pale pale kuhakikisha msimu ujao tunacheza mechi za kimataifa kwa kushika nafasi nne za juu," alisema.

Katika michezo hiyo, Dodoma Jiji imekusanya pointi tisa, ikishinda miwili, sare tatu na kupoteza miwili, ikikamata nafasi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, alisema wamerejea wakiwa hawana baadhi ya wachezaji ambao ni majeruhi, lakini wanaendelea vizuri na siku mbili tatu watajumuika na wenzao.

"Tuna Ibrahim Ajibu alipata majeraha katika mchezo dhidi ya Simba, halafu kuna nahodha wetu, Hassan Mwaterema naye ni mgonjwa, lakini hawa wote hali zao zinaendelea vizuri, tunaamini mpaka Ijumaa watakuwa wameungana na wenzao, hata kama hawakucheza mechi dhidi ya Coastal Union, basi watacheza mchezo unaofuata dhidi ya JKT Tanzania, Oktoba 29.

Katika mchezo wao wa mwisho kabla ya mapumziko, Dodoma Jiji iliishindilia Tabota United mabao 2-0.

## Simba kamili kwa dabi, Yanga yalia na muda

INATOKA UK. 24

walio kwenye kikosi cha Taifa Stars ambacho leo kinajitupa, Uwanja wa Benjamin Mkapa kucheza dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, Yanga pia imetoa wachezaji kwenye timu zingine za taifa, kama Stephane Aziz Ki, akiwa kikosi cha Burkina Faso, Kennedy Musonda na Clatous Chama, Timu ya Taifa ya Zambia, Khalid Aucho, akiichezea Uganda Cranes, na Djigui Diarra, akiitumikia Timu ya Taifa ya Mali.

Akiizungumzia presha katika mchezo huo kwa viongozi na mashabiki, Harrison alisema ni lazima iwepo kwani dabi ya Simba na Yanga ina hisia kubwa zaidi ya mchezo wenyewe wa soka.

Hata hivyo, alisema kwa viongozi hauwezi kuwapa presha kiasi cha kuzimia kama mashabiki au kusababisha kushindwa kutekeleza majukumu yao.

"Hata sisi viongozi tunakuwa na presha, kwani mechi za dabi ni za kihisia zaidi, huwa zinaenda mbali zaidi ya mchezo wenyewe wa soka, ila kwetu haiwezi kufikia hatua hiyo kama mashabiki kwa sababu unaweza kushindwa hata kutekeleza majukumu yako, hivyo ni lazima tuwe vizuri kwenye utimamu wa akili ili kuhakikisha tunatekeleza majukumu ya klabu, kama vile kuwaandaa vizuri kimwili na kiakili wachezaji, presha yetu haiwezi kuwa sawa na mashabiki," alisema.

Akielezea kama Kocha Mkuu Miguel Gamondi, amebadilisha aina ya mazoezi kuelekea mchezo huo, alisema mazoezi ni yale yale, ila wanachofanya ni kujiweka katika mazingira mazuri zaidi ya kiufundi kuhakikisha wanapata ushindi.

## Stars ni kufa kupona leo

INATOKA UK. 24

okuwapo uwanjani kuwapa hamasa wachezaji ili kuweza kupata ushindi.

"Ni kweli, Waziri Mkuu anatarajiwa kuwa mgeni rasmi kwenye mchezo wa kesho (leo), tunawaomba Watanzania wajitokeze kwa wingi kuwapa hamasa wachezaji kwa sababu ni mchezo muhimu zaidi kwetu, tunahitaji ushindi," alisema Ndimbo.

Kwenye msimamo wa kundi lao, DR Congo wanaongoza kwa kuwa na pointi tisa wakifuatiwa na Stars wenye pointi nne, nafasi ya tatu inashikwa na Guinea wenye pointi tatu huku Ethiopia wakiburuza mkia kwa kuwa kwa pointi yao moja.

Wakati Stars na DR Congo wakiumana leo kwenye mechi yao ya raundi ya nne, Ethiopia na Guinea zitaumana kesho kwenye mchezo wao wa marudiano wa hatua hiyo.

Michezo

Jumanne Oktoba 15, 2024

Nipashe

**Tchouamen hana mpango na Liverpool**

UKURASA 22



**PATASHIKA...**



Mshambuliaji wa England, Harry Kane, akiwania mpira na mchezaji wa Finland kwenye mechi ya Ligi ya Mataifa ya Ulaya, huku Jude Bellingham (kushoto) akiwa tayari kwenda kutoa msaada, kwenye mechi hiyo iliyopigwa katika Uwanja wa Helsinki Olympic, nchini Finland juzi. England ilishinda mabao 3-1. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA KAMILI KWA DABI, YANGA YALIA NA MUDA

## ●●●Kilio chao ni kwa wachezaji walioko timu za taifa, huku Fadlu akisema njooni sisi tupo...

**Faustine Feliciane na Adam Fungamwango**

WAKATI homa ya pambano la watani wa jadi, Simba na Yanga likizidi kupanda, Kocha wa 'Wekundu wa Msimbazi', Fadlu Davids, amesema wapo tayari kwa mchezo huo utakaopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumamosi, huku wapinzani wao wakilia na muda wa maandalizi kuwa mchache kwani watakuwa na siku mbili tu za maandalizi kwa nyota wao wengi walioko timu za taifa.

Simba na Yanga zitaumana Jumamosi ukiwa ni mchezo wa pili msimu huu ukitanguliwa na ule wa Ngao ya Jamii mwanzoni mwa msimu huu.

Akizungumzia mchezo huo, Fadlu alisema anaifahamu Yanga na ubora wake, lakini wamejiandaa kimkakati kuhakikisha wanapata ushindi kwenye mchezo huo.

Fadlu alisema kitu kikubwa ni kuwa na nidhamu ya mchezo, kutumia vizuri kila nafasi watakayoipata kufunga goli.

"Michezo kama hii inakuwa haina nafasi nyingi za kufunga, ni mchezo wenye upinzani mkubwa kutokana na aina ya timu zinazokutana, ni lazima sasa kutumia vizuri kila nafasi unayoipata, hiki ndicho ninachowasisitizia wachezaji," alisema Fadlu.

Alisema eneo lingine ambalo amewekea mkazo ni nidhamu ya kukaba kila wanapopoteza mpira.

"Yanga wana kikosi kizuri, wachezaji wake wamekaa pamoja muda mrefu, ni lazima tuwe na mikakati mizuri ya kukaba pale tunapopoteza mpira, ninaimani kubwa na wachezaji wangu," alisema Fadlu.

Kwa upande wa Yanga imesema itawaandaa kwa siku mbili tu wachezaji wake watakaorejea kutoka kwenye vikosi vya timu za taifa kwa ajili ya mchezo huo wa dabi.

Meneja wa timu hiyo, Walter Harrison, jana alisema kuwa wanategemea wachezaji wote wawe wamewasili kambini Jumatano, na watatumia siku mbili kati ya Alhamisi na Ijumaa kuwaweka vizuri kimwili na kiakili kwa ajili ya mchezo huo muhimu.

"Maandalizi yanaendelea vizuri kwa sehemu ya kikosi ambacho kiko Dar es Salaam, kama mnavyojua tuna kundi kubwa la wachezaji ambao wapo kwenye vikosi vya timu ya taifa, ila tunaamini kuwa wapo kwenye mikono salama na wanaendelea na maandalizi kuelekea kwenye michezo yao.

"Tunategemea wote watakuwa wamefika kambini Oktoba 16, kuelekea katika mchezo huo mkubwa na tarehe 17 na 18, siku hizo mbili tunazitumia kuwaweka vizuri kimwili na kiakili kwa ajili ya mchezo huo," alisema.

Harrison alikiri kuwa ratiba imebana sana kwani pamoja na yote itategemea wachezaji wao watarejea wakiwa katika hali gani kiafya.

"Ukiangalia ratiba ilivyo, na hawa wachezaji walio kwenye vikosi vya timu za taifa, hujui watarejea kwenye hali gani kiafya na kimwili, hivyo huwezi kutegemea nini kitatokea, lakini sisi tunaamini watarejea salama na tutakuwa kwenye wakati mzuri wa kukiandaa kikosi kuelekea kwenye mchezo huo muhimu kwetu kwani tunataka kuendeleza ushindi ili kuweza kuupata ubingwa mara ya nne mfululizo," alisema.

Mbali na kuwa na baadhi ya wachezaji

INAENDELEA UK. 23

# Stars ni kufa kupona leo

**Na Faustine Feliciane**

KAIMU Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars', Hemed Suleiman ,Moroco', amesema mchezo wa leo dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ni muhimu zaidi kwao kupata ushindi na watapambana kuanzia dakika ya kwanza mpaka ya mwisho kutimiza lengo hilo.

Katika mechi hiyo ya marudiano kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika mwakani nchini Morocco, itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, majira ya saa 10:00 jioni, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitarajiwa kuwa mgeni rasmi na kuongoza hamasa kwa wachezaji wa Taifa Stars ili kuweza kupata ushindi.

Akizungumzia mechi hiyo, Morocco alisema baada ya kupoteza mchezo wao wa kwanza dhidi DR Congo wiki iliyopita ugenini jijini Kinshasa, huku pia Guinea ambao wapo nao kundi moja wakipata ushindi dhidi ya Ethiopia, mchezo wa leo ni muhimu zaidi kwao kupata ushindi.

"Ingawa bado kuna michezo mingine mbele yetu, lakini mchezo wa kesho (leo), ni muhimu sana kwetu ili kuendelea kuweka hai malengo yetu ya kufuzu kwa fainali za Afcon, naamini tunauwezo wakupata ushindi nyumbani," alisema Morocco.

Aidha, alisema licha ya kufungwa kwenye mchezo wao wa kwanza, bado timu yake ilicheza vizuri na ana matumaini leo kuibuka na ushindi kwenye uwanja wao wa nyumbani.

Nahodha wa timu hiyo, Mbwana Samatta, alisema wachezaji wapo tayari kwa ajili ya mchezo huo na wao watautumia vizuri uwanja wao wa nyumbani.

"Benchi la ufundi na sisi wachezaji wote, akili zetu zipo kwenye mchezo huu, tutapambana kama wachezaji kuhakikisha tunapata ushindi na kuwafurahisha Watanzania, tupo tayari kwa ajili ya mchezo huu wa marudiano," alisema Samatta.

Wakati huo huo, Ofisa Habari wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, alisema Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, anatarajiwa kuwa miongoni mwa Watanzania wataka-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >